

Roho Zinazoshawishi

 Habari za asubuhi, marafiki. Nina furaha kuwa hapa asubuhi ya leo, na nikijua ya kwamba ninaona ninyi nyote mmetoka, nikiamini ya kwamba Bwana yuko pamoja nasi leo, akitupa kivuli kidogo cha namna fulani, hivi kwamba hapatakuwa na joto sana hapa maskanini kwa ajili ya ibada ya asubuhi. Na sasa tu . . .

² Ninaamini, je! kuna watoto . . . Watoto wameruhusiwa kuondoka kwenda kwenye madarasa yao, Ndugu Neville? Nimeona baadhi ya watoto. Nilishangaa kama wameruhusu madarasa yarudi kwenye ninii yao—vyumba vyao vingine, kwenye chumba chao cha shule ya Jumapili.

³ Sasa, niombeeni. Nina uamuzi mkubwa nilipaswa kufanya jana usiku, nami sina budi kuufanya leo. Na hebu kanisa liombe. Ninam—nina mkutano unaokuja usoni, kule kule kabisa kwenye Ngome ya Pazia ya Chuma huko Ujerumanii, na kwa hiyo ni nyeti kidogo. Na mniombee. Na kwa hiyo, ni, twaweza kuanza mara moja kwenye ule uwanja wa mpira wa kriketi huko Ujerumanii, ambaao Hitler aliujenga kabra tu ya vita, mahali pakubwa pazuri, panakaa watu elfu themanini. Nasi tunaweza kupatumia kwa siku kumi usiku, mfululizo. Basi tunatarajia kuanza huko mara moja, na halafu twende huko La Salle Lorraine, Ufaransa, baadaye, kisha hadi Berlin, turudi . . . ninamaanisha, Berlin kati ya hapo na—na Ufaransa.

⁴ Kisha tatarudi, Bwana akipenda, kwenye mkutano huko Chicago. Unaanza, nafikiri, tarehe tano, sita, saba, nane, na tisa, ni wilaya yangu ya Chicago, ya ule mkutano kwenye— kwenye kanisa la Kiswidishi. Halafu wanainii, Bw. Boze, baadhi yenu kutoka karibu na Chicago, wana mkutano uliokuwa unakuja ninii hii ifuatayo . . . kuanzia Agosti moja, ama Septemba moja, kwenye wakati huo, huko Swideni. Nami nina furahi sana kujua ya kwamba kura zao walizonipigia, ili niende huko, na ilipitishwa na watu wote na zilikuwa asilimia moja. Nilifurahia jambo hilo, lakini sina budi aidha kwenda kule ama nishuke hapa sasa. Ninyi ombeni ya kwamba Bwana ataniongoza moja kwa moja kabisa hadi mahali pale ambapo watu wengi wataokolewa, na lile lililo bora sana litafanywa kwa ajili ya Ufalme wa Mungu. Sasa, wao wana mkutano kule juu, na—na wao huko Swideni, naye alisema tungekuwa na watu elfu ishirimi na tano, thelathini na tano kwanza, kwenye huo mkutano, na wengi wao ni watu ambaao hawajaokoka.

⁵ Na halafu ukishuka hapa Ujerumanii, vema, wana kiwanja kinacho kaa watu elfu themanini. Bila shaka, sisi, kule Switzerland ambako ndiko tunakotokea, tulikuwa na mkutano

mzuri sana huko, na wengi wenu labda hamjasikia bado. Bwana alitubariki vya ajabu sana, tulipata waongofu elfu hamsini katika siku tano usiku, huko—huko—huko Zurich, Switzerland.

⁶ Na kwa hiyo, Ndugu Jack Shuler, wengi wenu mnajmua, yeeye ni Mmethodisti, kijana wa mzee Bob Shuler. Wao wako Belfast sasa, na—nao wanasema wanapapindua mahali hapo, kwa ajili ya Injili, na hata zaidi ya vile Billy Graham alivyofanya katika mukutano wake. Jack ni kijana mdogo mzuri sana, amejaa bidii na upendo. Na yeeye—yeeye ni mwaminifu sana kwa hilo hata ninaamini yeeye ni mtumishi mkuu wa Bwana. Nami ninamwombea Ndugu Shuler. Na—na ilikuwa ni Jack Shuler, na Jack MacArthur pia yuko pamoja naye. Ndugu Jack MacArthur ni mhubiri mkubwa, pia. Na kule watu wa kanisa wamesema ndio mukutano wa ufufuo ulio mkuu sana uliopata kuingia Ireland. Kwa hiyo tunaninii sana... Ingieni kwenye maombi kila siku kwa ajili ya watu hao. Wote wawili ni vijana, chini, karibu miaka arobaini, nakisia, ama chini yake, familia na kadhalika, na waalimu wazuri na thabiti wa Injili, nasi tunawapenda.

⁷ Na sasa, na-naomba ya kwamba hamtanisahau mimi, ya kwamba, na Mungu atanijalia kutoa uamuizi mzuri sasa hivi. Kuna nyakati ambapo hujuu uelekee wapi. Ulipata kuingia katika hali kama hizo? Ninaamini Paulo alipata kufikia mahali kama hapo wakati mmoja, sivyo? Ilikuwa kati ya njia mbili. Na wakati alipokuwa akivuka aende kule, mbona, aliona malaika katika ono ambaye alimwambia, "Njoo huku Makedonia." Kwa hiyo Bwana angali ana Malaika Wake, sivyo? Kama ningeweza tu kuwa mnyenyeketu moyoni mwangu kuhusu jambo hilo kama alivyokuwa Paulo.

⁸ Na sasa, usiku wa leo, kumbukeni ibada za Injili hapa maskanini, kila mtu na aje. Ninyi mlion karibu na Louisville, nitahubiri kwenye kanisa la Mlango Uliofunguliwa, usiku wa leo, kwa masaa kadha, saa moja na nusu hadi saa tatu na nusu, kwa Ndugu Cobbles. Nilikuwa nije hapa mara mbili. Halafu yeeye ni mtu mzuri sana, naye akapiga simu. Naye Ndugu Cobbles, yeeye ni ndugu muungwana sana. Ninyi, nina hakika mnajmua, ndugu mzuri sana, na ilikuwa ni vigumu kumkatalia kirahisi hivyo. Ombeni. Juu ya yote, ombeni, tena ombeni ya kwamba Mungu atatupa kufanya u—uamuizi mzuri.

⁹ Sasa, kabla hatujaanza Ujumbe wa Injili, tuna asubuhi tutakayowaweka watoto wadogo wakfu. Nami nina jamaa mdogo hapa wa kuweka wakfu, pia, kwa Bwana. Sasa, wakati mwingi katika makanisa mengi...

Mnaweza kusikia vizuri, huko nyuma kabisa? Kama mnaweza, ni sawa? Hizi feni hapa, mimi ninaninii tu, huwezi kujisikia wewe mwenyewe. La, hiyo, hiyo ni sawa. Ninaogopa nitaangamia bila hiyo.

¹⁰ Kwa hiyo wa—watoto wadogo, wakati mwininge wanawanyunyizia, kanisani, wakati wao ni watoto wachanga sana. Na, bila shaka, jambo hilo linatokana na kanisa Katoliki, kwa kuwapa hao watoto majina ya kidini, ama “kuwabatiza” kama wanavyowaita wakati wakali ni watoto wachanga. Kanisa la Kimethodisti likaleta jambo hilo, hilo la ubatizo wa watoto wachanga na mengi, na nafikiri mengine mengi. Nafikiri hiyo ndio tofauti kati ya la Wanazarayo na Wamethodisti wa mtindo wa kale, ilikuwa ni ubatizo wa watoto wachanga, halafu vile vikundi vilivyojitenga na kadhalika. Lakini, kwa njia yo yote ile, haininii, sidhani ni la muhimu sana. Kwa sababu, hata hivyo, nafikiri Kalvari iliondolea mbali jambo hilo, papo hapo, kwa yote hayo, maana Yesu alikufa pale apate kuwaokoa watoto wadogo na kuuokoa ulimwengu.

¹¹ Na mtoto mdogo, haidhuru ana wazazi wa namna gani, ni wenye dhambi namna gani, hilo halingeleta tofauti yo yote, kwa maana Damu ya Yesu Kristo humsafisha, unaona, na huyu ni Mwana Kondoo wa Mungu aichukuaye dhambi ya ulimwengu. Mtoto huyo mchanga hawezi kutubu. Hajui jinsi ya kutubu. Hajui sababu ya kuwa hapa, kwa nafsi yake mwenyewe. Hawezi kujuua ni kwa sababu gani ye ye yuko hapa. Lakini Mungu alimleta hapa, nayo Damu ya Yesu Kristo inamsafisha wakati ule ule anapoingia ulimwenguni. Na ni mpaka amefikia umri wa kuwajibika, ndipo anapojua mema na mabaya, na ndipo analofanya hana budi kutubu kwa jambo analogua ya kwamba amefanya mabaya. Hiyo ni kweli. Kwa hiyo, wengine wao huwanyunyizia, nao wanafikiri hawaendi Mbinguni.

¹² Na kuna fundisho linalosema kama mtoto mchanga amezaliwa na wazazi wenye Roho Mtakatifu, vema, mtoto huyo mchanga ataenda Mbinguni; lakini, kama hajazaliwa nao, amekwisha, mtoto huyo mchanga ameangamia. Hilo ni kosa kabisa. Inaleta tofauti gani kama ni wazazi walio na Roho Mtakatifu? Jambo lote ni tamaa ya kujuana kimwili, na mtoto mchanga anazaliwa kwa jinsi ile ile. Kwa hiyo, wote “wanazaliwa katika dhambi, wanaumbika katika uovu, wanakuja ulimwenguni wakisema uongo.” Hayo, hayo ni maneno ya Maandiko ya jambo hilo.

¹³ Kwa hiyo, na ndipo Damu ya Bwana Yesu inasafisha na kufanya upatanisho kwa ajili ya mtoto huyo. Kama akifa, angeenda moja kwa moja katika Uwepo wa Mungu, kama alizaliwa kutokana na wazazi walio wazinifu sana ulimwenguni, mpaka afikie umri wa kuwajibika ambapo anajua mema na mabaya. Halafu lile atendalo, tangu wakati huo, hana budi kusamehewa kwa jambo hilo. Hana budi kujiombea msamaha mweneyewe tangu wakati huo na kuendelea. Lakini wakati ye ye angali ni mtoto mchanga . . .

¹⁴ Sasa, jinsi tunavyojaribu kufuatilia jambo hilo, hapa maskanini. Ndipo mahali pekee ulimwenguni ninapoenda,

ninahubiri Mafundisho, ni hapa maskanini, kwa sababu, hili ni kanisa letu. Nasi tunahubiri Mafundisho hapa kuwaweka watu sawa. Watu wengine, katika makanisa yao, wanahubiri cho chote wanachoamini. Nao ni ndugu zangu, nasi tunaweza tukatofautiana kidogo, lakini sisi tungali ni ndugu vile vile tu. Na, lakini hapa maskanini, tunahubiri kile tunachoona ni Fundisho la Kimaandiko. Na, humo ndani, tunaona kuhusu kuwekwa wakfu kwa watoto, kile tunachoita kuwekwa wakfu, wakati pekee katika Biblia ambapo tunaweza kuona, ama ambapo katika Agano Jipyä ambapo watoto wadogo waliwahi kuwa na uhusiano wo wote, ama Kristo alipata kuwa na uhusiano wo wote na jambo hilo katika sherehe, ilikuwa, Yeye aliwachukua mikononi Mwake na kuwawekea mikono na kuwabariki, na akasema, "Waacheni watoto wadogo waje Kwangu. Msiwakataze, kwa maana Ufalme wa Mungu ni wao."

¹⁵ Sasa, tumeachiwa, kama tunavyofahamu, kuendeleza kazi ambayo Yeye alikuja ku—kumalizia. Mauti Yake pale Kalvari, Yeye alikuwa pamoja nasi Naye alitoka kutoka... alitoka kwa Mungu, akaja ulimwenguni, akarudi kwa Mungu, ama kutoka ulimenguni akarudi kwa Mungu, kisha akarudi tena katika umbo la Roho Mtakatifu, naye yuko pamoja nasi, ndani yetu, hata ukamilifu wa dahari, akiendeleza katika Kanisa Lake kazi zile zile ambazo alizifanya alipokuwa hapa duniani. Na, kwa njia hiyo, tunawachukua watoto wetu mmoja kwa mwingine, kwa wahudumu, nao wanawaombea, wanawekea mikono yao juu yao na kuwaweka wakfu kwa Mungu. Sherehe ndogo tu ya kusema ya kwamba tunathamini yale Bwana aliyotufanya sisi pamoja na watoto wadogo.

¹⁶ Sasa, kama mtoto wako mdogo ameshanyunyiziwa maji, ama cho chote kile ilivyo kanisani mwenu, wazia. Hatusemi neno lo lote dhidi ya jambo hilo. Vema. Lakini, Kimaandiko, tunaona tu mahali pamoja, hapo ni pale ambapo Yesu aliwabariki, Yeye Mwenyewe. Hayo nitayasoma, Bwana akipenda, ka—katika Neno hapa. Tunaona, katika Luka Mtakatifu ile... ninaami ni—ni sura ya 10, na kuanzia aya ya 13.

*Wakamletea na watoto wachanga ili awaguse;
lakini wanafunzi Wake walipoona waliwakemea wao
waliowaleta.*

*Bali Yesu alipoona alichukizwa sana, akawaambia,
akawaita waje kwake, akasema, Waacheni watoto
wadogo waje kwangu, wala msiwazuie; kwa kuwa watu
kama hao ufalme wa Mungu ni wao.*

*Amin, nawaambia, Mtu ye yote asiyeupokea ufalme
wa Mungu kama mtoto mdogo hauingii kamwe.*

*Akawakumbatia, na akaweka mikono yake juu yao
akawabarikia.*

¹⁷ Ni zuri sana? Akasema, "Sasa, waacheni watoto wadogo waje Kwangu. Msiwakataze, kwa kuwa watu kama hao, watu walio kama mtoto huyo mdogo, Ufalme wa Mungu ni wao." Ndipo akawakumbatia akawabarikia.

¹⁸ Sasa, jinsi tungalipenda, asubuhi ya leo, kama tungeweza kuwa na Yesu ameketi Yeye, Mwenyewe, hapa jukwaani, useme, "Bwana, utambariki mtoto wangu?" Loo, ni ninii... kwa macho yetu ya kibinadamu na mioyo yetu ikitamani sana kuona hilo. Lakini ye ye yuko hapa, hata hivyo, kwa maana Yeye alitupa agizo kufanya jambo hilo. Na, kama tulivyofanya, basi Yeye hutambua. Tunapowapokea wale aliquota, tunapokea Yeye aliyempeleka, manaona. Kwa hiyo, Yeye yuko hapa asubuhi ya leo. Na kama Dada Gertie atakuja hapa kwenye piano na kupiga ule wimbo wetu wa zamani tuliozoea kuimba muda mrefu uliopita, huu, "Walete, walete watoto wadogo kwa Yesu." Ninaamini uko kwenye kitabu pale mahali fulani. Sina hakika. "Walete watoto wadogo kwa Yesu." Na kama una mtoto mchanga ambaye hajawekwa wakfu bado, nawe unataka kumweka wakfu asubuhi ya leo, mbona, tutafurahi kufanya jambo hilo.

¹⁹ Na kuna wahudumu wo wote humu jengoni, wahubiri ambao wangependa tu kuja na kusimama pamoja nasi hapa tunapowaweka wakfu hawa watoto kwa Bwana? Tutafurahi kuwa pamoja nanyi, mnapokuja. Vema, uko kwenye hicho kitabu hapo? Umeupata, Ndugu Neville? Haupo. Vema, ni wangapi wanaujua, *Walete?* Vema, na tuuimbe sasa. Kila mtu pamoja, wakati akina mama wanapowaleta watoto wao wachanga. Vema. Vema.

. . . lete, walete,
Kutoka dhambini walete,
Walete, Walete,
Na walete Kwake Yesu.

Walete, Walete,
Kutoka dhambini walete,
Walete, walete,
Na walete Kwake Yesu.

²⁰ Na tuinamishe vichwa vyetu kidogo. Baba yetu wa Mbinguni, akina mama na akina baba wamesimama madhabahuni asubuhi ya leo wamewakumbatia watoto wao mikononi mwao, ambao Wewe umewapa kwa neema. Wanashukuru sana kwa ajili yao, Bwana, nao wanawaleta hapa madhabahuni asubuhi ya leo, katika nyumba ya Mungu, kuwaweka wakfu, kuyatoa maisha yao Kwako. Wewe umewapa. Nasi tunaomba, Mungu, ya kwamba utawalisha na kuwabariki kila mmoja wao. Waongoze, na jalia Malaika walinzi wa Mungu wamlinde kila mmoja wao. Wape maisha marefu ya heri na furaha. Na wakue wapate kuwa wanaume na wanawake wa Mungu, wa kesho, kama kuna kesho.

²¹ Ee Mungu, tunaomba ya kwamba Wewe utainua wahubiri na manabii na waalimu kutoka katika kundi hili la watoto wachanga linalozunguka madhababu hii asubuhi ya leo. Nasi tutakapokuwa wazee na hatuwezi kuendelea mbele tena, mtu fulani hana budi kutupeleka mahali hadi mahali, jalia tuweze kusimama na kuisikia Injili ikihubiriwa na hawa walio hapa leo. Tujalie, Bwana. Na siku moja yenye utukufu wakati yote yatakapokwisha, maisha yetu yamekwisha, wazazi hawa waliopo madhabahuni, jalia tuwe kama Yakobo wa kale wakati alipowabariki watoto wake wote na kuwaambia mwisho wao utakuwa ni nini katika siku za mwisho. Ndipo aliangalia juu, akasema, “Mnajua, sina budi kukusanya pamoja na watu wangu.” Na siku moja yenye utukufu, ye ye pamoja na watoto wake wote, watakusanya pamoja katika nchi iliyo bora zaidi. Si ajabu Balaamu alisema, “Jalia mwisho wangu uwe kama wake.” Mungu, naomba ya kwamba utawajalia wazazi hawa baraka hizi.

²² Na sasa tunapoenda kuweka mikono yetu juu yao, ni—ni ajabu... Na jinsi uliviyolifanya jambo nyenyekevu, Bwana, ya kwamba sisi watu wa dunia hii tungekuwa na majaliwa ya kuwabariki watoto wadogo katika Jina Lako, tukijua jambo hili, ya kwamba, tuombalo, tunajaliwa. Tunapoenda kuwabariki, jalia Yesu, Mtu asiemeonekana, Yeye mwenye nguvu zote asimame karibu na kumbariki kila mtoto tunapoiweka mikono yetu juu yao na kuwatoa Kwake. Kwa maana tunaomba katika Jina Lake. Amina.

²³ Ndugu Glenn Funk, ye ye ana watoto wake wadogo watatu wa kuwekwa wakfu kwa Bwana.

[Mahali patupu kwenye kanda. Ndugu Branham anawaweka watoto wakfu—Mh.]

Wewe huko mbali katika kibanda ki—kidogo, cha kale, katika nchi ya kaskazini, uliniahindi mtoto huyu. Baba, naomba baraka Zako zikae juu yake.

Joseph, kijana wangu, ninakutoa kwa Mungu. Na naomba maisha yako yawe na baraka. Naomba uwe nabii, Joseph. Neema ya Mungu na ikae juu yako. Mungu wa baba yako, Bwana Yesu Kristo, na akubariki, na ayafanye maisha yako kuwa ya baraka kwa wengine.

Katika Jina la Yesu Kristo, ninambariki. Amina.

[Mahali patupu kwenye kanda. Ndugu Branham anawaweka watoto wachanga wakfu—Mh.]

²⁴ Mnawapenda watoto wadogo? Jambo fulani juu ya watoto wadogo ambapo kila mama anataka mtoto wake abarikiwe.

Sasa, hivyo ndivyo Baba yetu wa Mbinguni alivyo kwetu sisi watu wazima asubuhi ya leo. Anataka kila mmoja wetu abarikiwe. Yeye hutupeleka mbele ya jambo fulani,

anatupa tu jambo hilo, kama kusema, "Angalia, nakutaka ubarikiwe, mwanangu." Yeye si ni wa ajabu? Kwa hiyo tunaweza kumthamini Baba wa Mbinguni mwenye huruma kama huyo.

²⁵ Sasa, katika kule kuwabariki watoto wachanga, mnajua, nilikuwa tu nikisoma hapa katika Maandiko juzijuzi, mahali fulani hapa, ilikuwa ni katika Agano la Kale, ambapo ja-jambo kuu ambalo bila shaka ni-nililifurahia kulisoma. Hili hapa, papa hapa. "Nathanaeli akamwambia Daudi, 'Fanya yote yaliyomo moyoni mwako, maana Mungu yu pamoja nawe.'" Unaona? Fanya yale yaliyomo moyoni mwako. Na mara nyingi ni-nimeona jambo hili, rafiki yangu Mkristo, kwamba nimesema mambo bila kujua yale ningesema, na kuja kutambua yametimia! Utakalosema!

²⁶ Ilisemwa wakati mmoja, Yesu alishuka kutoka mlimani na kuona mti usiokuwa na kitu, ni majani tu, wala hakukuweko na matunda, ndipo akasema, "Tangu leo mtu asile matunda kwako."

²⁷ Na kesho yake, alipokuwa anapita hapo, wale mitume wakaona matawi yamenyauka. Akasema, "Jinsi gani mti umenyauka mara."

²⁸ Yesu akasema, "Mwaminini Mungu; maana yo yote mtamaniyo, mkisali, aminini ya kwamba mnayapokea nayo yatakuwa yenu. Na yo yote msemayo, mtapokea usemayo." Wazia jambo hilo. Loo! Na labda leo, Roho Mtakatifu mkuu wa Mungu, akiwa amesimama hapa madhabahuni, mnasema... Vema, si lazima ipambwe. Si lazima pawe ni mahali palipotiwa madoido mengi.

²⁹ Yakobo alivuta jiwe wakati mmoja na kulaza kichwa chake juu yake, na lingali linatambuliwa leo kama Jiwe la Kuvishia Taji. Ama Jiwe la Kuvishia Taji, ambalo watu wakuu wa ulimwengu wangali wanalibeba jiwe hilo kila mahali, kusudi wafalme watawazwe juu ya jiwe hili, jiwe tu la kawaida la zamani la kondeni.

Betheli ulikuwa ni lundo la miamba iliyolundikana, nayo ikawa nyumba ya Mungu, mahali pa kukaa. Yakobo alisema, "Hapa si mahali pengine ila ni nyumba ya Mungu." Lundo la mawe limewekwa moja juu ya lingine.

³⁰ Haihitaji mambo yenye madoido sana. Inataka urahisi na imani ya kuamini, ndicho kinachohitajika. Hiyo ndiyo ishindayo.

³¹ Sasa, tukijua ya kwamba wakati karibuni unaisha, tutajaribu kutowaweka kwa muda mrefu sana, tukijua kuna joto na kanisa limejaa watu. Kwa hiyo nitazungumza nanyi kwa muda kidogo tu asubuhi ya leo, juu ya somo dogo hapa ambalo linaweza... Ninatumaini litakuwa ni msaada kwenu. Na sasa mimi, kabla sijaondoka nyumbani, niliandika mambo mdadogo matatu ama manne. Nikasema, "Nitangojea nione yale

Bwana atakayoniruhusu kunena nitakaposhuka kwenda kule.” Niliandika mambo madogo sita hivi hapa, masomo madogo, nami nikaandika moja, nikaliweka mfukoni mwangu namna hii. Nikawaza, “Vema, nitakapoenda mimbarani labda ataniambia jambo la kuzungumzia.” Sasa niko tu mbali kama nilivyokuwa kule. Kwa hiyo, hata hivyo, nitasoma Andiko fulani hapa, Bwana na atusaidie kulielewa. Sura ya 14 ya Luka Mtakatifu, na hebu tuanzie kwenye thela . . . aya ya 31 ya sura ya 14 ya Luka Mtakatifu.

Au kuna mfalme gani, akitaka kwenda kupigana na mfalme mwingine, asiyeketi kwanza na kufanya shauri, kwamba ye ye pamoja na watu elfu kumi ataweza kukutana na yule anayekuja juu yake na watu elfu ishirini?

Na kama akiona hawezi, ama ye ye ni . . . hutuma ujumbe kutaka sharti za amani, mtu yule akali mbali.

Basi, kadhalika kila mmoja wenu . . .

³² Sasa nawatakeni mchunguze kwa makini. Sasa, kwanza Yeye alisema . . . Ni mfano. Alisema, “Sasa, kuna mfalme anayekuja, naye ana wanajeshi elfu ishirini; na mfalme *huyu* anaenda kukabiliana naye, naye ana wanajeshi elfu kumi tu. Kwa hiyo basi, kwanza, anaketi chini na kuuliza kama ye ye yuko tayar, kama anaweza kufanya jambo hilo ama hawezi.” Vema.

. . . kila mmoja wenu asiyearcha vyote alivyo navyo, hawezi kuwa mwanafunzi wangu. (Mnaona?)

³³ Sasa Bwana na aongeze baraka Zake kwenye Neno hili. Sasa hebu na tuinamishe vichwa vyetu kidogo.

³⁴ Baba yetu wa Mbinguni, Wewe unayejua mambo yote, wala hujali utu wa mwanadamu, kwa kuwa mwanadamu ni nani hata umjali? Ulimfanya mwanadamu, naye ni kama tu ua la uwandani: leo ni zuri, kesho limekatwa, na kutupwa jikoni, nalo hunyauka. Nami nakuomba Wewe, Mungu, uturehemu leo na utujalie kila mtu ajichunguze leo. Tuko hapa kama katika nyumba ya masahihisho. Tuko hapa kujifunza jinsi ya kuishi, na jalia litoke kwenye Neno Lako leo, Ee Mungu wa Milele. Wengi wa watoto Wako wamekusanyika, na wengi wao wamekuwa ni watoto Wako kwa miaka mingi, lakini, kama hao, sote tunarudi katika nyumba ya Mungu, kujifunza, kujua. Nami, mtumishi Wako, ninatamani kukujua Wewe zaidi. Nami naomba ya kwamba utaleta upako wa Injili juu yetu sote, juu ya mtumishi Wako, na ya kwamba Uwepo Wako na kutuvuyia katika jengo hili kutakuwa kukuu sana leo, hata tutaondoka, katika moyo wetu, tukitamani kuwa watumishi Wako bora zaidi, ili kwamba liwe jambo la manufaa kwetu kuwepo hapa. Ee Mungu mwenye rehema, tujalie baraka hizi, katika Jina la Yesu, Mwanaao. Amina.

³⁵ Sasa Bwana na aongeze baraka Zake kwa Neno Lake tunapolisoma. Ninataka kuchukua fungu la maneno asubuhi ya leo, ambalo, "Roho zinazoshawishi ama Neno la Mungu?" Sasa, kwa namna fulani ni somo geni, lakini kwa kuwa ni kwenye maskani... Na Jumatano usiku... Jumapili iliyopita asubuhi nilikuwa nikizungumza juu ya yubile ndo—ndogo ya Injili.

³⁶ Na usiku wa Jumatano iliyopita nilikuwa nikihubiri juu ya yule mwanamke aliyekuwa na ile—ile dusumali kichwani mwake, ama ninii... Yeye alipoteza mojawapo ya sarafu zake, naye alikuwa akifagia nyumba na kujaribu kuipata kabla mumewe hajarudi. Ndipo tukaja kukuta kwamba mwanamke huyo alikuwa ni mwanamke wa kimashariki, naye... naye aliwakilisha Kanisa. Na dusumali ya arusi ilikuwa haivaliwi kwenye kidole. Ilivaliwa kichwani, ikiwa na vipande tisa vya fedha. Na wakati mwanamke alipokuwa kahaba, waliondoa kipande kimoja cha fedha na kuonyesha kwamba alikuwa kahaba. Na kwa hiyo mwanamke huyu alikuwa amepoteza moja ya vile vipande, si kahaba. Lakini mumewe alikuwa safarini, naye alikuwa akijaribu kuharakisha kupata kipande hicho, kukirudisha kwenye dusumali yake, kwa kuwa mumewe atakapokuja angejua ya kwamba ye ye alikuwa ameshikwa katika ukahaba, na ingemaanisha kuvunjika kwa nyumba na kadhalika. Nami nilitumia jambo hilo kwa dakika chache kwa kanisa, limepoteza mambo mengi makuu. Na wakati wa Baba kuja umewadia, kwa hiyo hatuna budi kuvitafuta. Sasa, nikijua kanisani, na maskani yetu...

³⁷ Nami—nami ninataka kuzungumza juu ya *Roho Zinazoshawishi*, ambalo kweli lingeitwa *Elimu Juu ya Pepo*. Mnasikia mambo mengi sana juu ya pepo, za siku hizi, lakini mnasikia machache sana juu ya jinsi ya kuziondoa. Sisi sote tuna—tunajua ya kwamba kuna pepo, lakini, jambo lingine ni, jinsi ya kuondoa kitu hicho. Na sasa kuna ninii... Nikiwa nimekuwa, kwa neema ya Mungu, na nafasi nyingi za kushughulika na vitu hivi vinavyoitwa pepo, na kukutana nao jukwaani na katika maisha ya kila siku, na, mbona, ningetaka kuangalia kwenye Maandiko asubuhi ya leo, na kuona vitu hivyo ni nini basi.

³⁸ Sasa, tuliiatumia katika ibada ya uponyaji, daima kwenye upande wa uponyaji. Kansa, vivimbe, mtoto wa jicho, kifua kikuu, vitu hivyo vyote si mambo ya kawaida, ni ya kiroho na ni pepo. Maandiko yanathibitisha jambo hilo dhahiri. Lakini hao ni pepo mwilini, pamoja na vivimbe, kama kansa, vina uhai ndani yake, na uhai wake ni pepo. Kivimbe cha mtoto wa jicho, kuenea kwa ugonjwa wa kifua kikuu, na magonjwa mengine, ni pepo. Hiyo ni katika maumbile ya mwili.

³⁹ Sasa, asubuhi ya leo tutazungumza—tutazungumza juu ya pepo katika umbo la kiroho kwenye nafsi. Wako kwenye nafsi jinsi ile ile tu walivyo katika mwili. Nasi inatubidi kukubali ya

kwamba tunawaona katika miili ya watu, kama vile kansa na—na magonjwa mbalimbali yaliyo katika miili ya binadamu.

⁴⁰ Hivi karibuni tu, hata kansa imetangazwa kwamba ni ugonjwa wa kiwango cha nne, kwamba uko katika kiwango kingine. Hakika, ni elimujuu ya pepo. Kila ugonjwa ni ugonjwa wa kiwango cha nne, mwanzo wake.

⁴¹ Sasa, lakini sasa kansa katika mwili ama kansa katika nafsi, pepo anaweza kuja katika mahali pote pawili. Sasa, kuna mara nydingi na watu wengi wenyewe mawazo mazuri kwamba...na watu wazuri wanaajaribu mara nydingi ku—kushikilia theolojia ndogo waliyo nayo, ama jambo fulani ambalo wamefundishwa tangu utotonii, na bado wanaona ya kwamba ndani kabisa ya utu wao, ndani kabisa ya nafsi yao, wangali wana jambo ambalo si sahihi. Ninyi, wengi wapo hapa asubuhi ya leo, hapana shaka mahali po pote unapowakuta Wakristo wamekusanyika pamoja, unawakuta watu walio na roho kama hizo ndani yao, ya kwamba wao... Hazifai. Hawazitaki. Wao wanasema, “Loo, laiti ningaliacha tu kusema uongo! Laiti ningaliacha tu kutamani! Laiti ningaliacha tu *hili* ama *lile!*” Sasa, hao ni pepo. Na, sasa, wao wanakuja katika mfano wa dini, mara nydingi. (Kwa kuwa ni shule ya Jumapili, ni wakati wa mafundisho, kwa hiyo hebu na tuangalie jambo hili.) Sasa, wao wanakuja katika mfano wa dini, mara nydingi.

⁴² Sasa, katika Maandiko, wakati mmoja, kulikuweko na mtu aliyeitwa Yehoshafati, mtu mkuu, mtu wa dini. Naye akaenda kwa mfalme mwengine ambaye alikuwa ni mfalme wa—wa Israeli. Naye, Yehoshafati, akiwa ni mfalme wa Yuda. Ndipo akashuka akaenda kwa Ahabu, mfalme wa Israeli, nao wote wakaungana pamoja, na kufanya mapatano, waende wakapigane huko Ramoth Gileadi. Nao walifanya jambo hilo bila kuomba kwanza.

⁴³ Loo, laiti watu wangalitambua! Hiyo ndiyo sababu nilikuja asubuhi ya leo na kuwaomba mnikumbuke ninapoenda katika nchi za ng'ambo. Katika mambo yote, ombeni!

Mtu fulani alikuja hivi majuzi akasema, “Ndugu Branham, unafikiri ni vibaya kufanya jambo fulani?”

⁴⁴ Nikasema, “Kwanini unaniuliza?” Unaona? Kama kuna swali moyoni mwako, liache, usilifanye jambo hilo kamwe. Dumu na hilo tu. Unapoanza kufanya jambo lo lote, na iwapo ni swali kama ni zuri ama baya, liache. Usiliingilie hata kidogo, ndipo utajua ya kwamba uko sahihi.

⁴⁵ Sasa, mambo yote yanapaswa kufikiriwa kwa maombi, kwanza. “Utafuteni kwanza Ufalme wa Mungu na haki Yake, na mambo haya mengine yote mtazidishiwa.” Nina hakika kabisa asubuhi ya leo, kama wanaume na wanawake wangeweza kufikia mahali ambapo nafsi yao, mawazo yao, na mwelekeo

wao, utakuwa mkamilifu mbele za Mungu, hilo lingekuwa moja ya makanisa yenye nguvu sana yaliyopata kuwepo.

⁴⁶ Angalia kwa dakika chache kwenye mambo ya maumbile ya kimwili. Sasa, tunanini, tumekuwa, mara nyigi, tumekuwa kwa miaka mingi, tuna chombo kinachoitwa “kigundua uongo.” Unaweza kukiweka kwenye kiwiko chako, wakiweke kichwani mwa—mwao, nawe unaweza kuingia mle na kujaribu uwezavyo kuufanya uongo usikike kama ni kweli, na kitakanusha kila wakati, kwa maana mwanadamu hakufanywa apate kudanganya. Uongo ni kitu kidanganyifu, kigumu, kiovu. Afadhalii niwe na mlevi, siku yo yote, kuliko mwongo. Unaona? Mwongo! Na mwili wako haukufanywa upate kusema uongo. Hata uwe mwenye dhambi namna gani, ungali u mwana wa Mungu aliyeanguka. Mtu mwenye dhambi sana kuliko wote humu mjini leo, Mungu hakukusudia wewe uwe mwenye dhambi. Yeye alitaka kukufanya wewe kuwa mwana ama binti Wake. Umeumbwa kwa sura Yake Mwenyewe. Lakini dhambi imekufanya ufanye jambo hilo. Na haidhuru unajaribu kuiga namna gani na kujaribu kufanya uongo uonekane kama kweli, wana chombo cha kisayansi kinachothibitisha ya kwamba ni uongo. Unaweza kuusema kwa usafi wo wote unaotaka, lakini kingali kitakanusha; kwa sababu kuna dhamira ya ndani katika mwanadamu, na dhamira hiyo ya ndani inajua kweli. Na hata useme nini kule nje, hiyo dhamira ya ndani inajua ya kwamba ni uongo, na itaandika kutoka kwenye dhamira hiyo ya ndani.

⁴⁷ Kwa hiyo, kama mwanamume ama mwanamke wakiwahi kuweka mawazo yao, na ushuhuda wao na maisha yao yamewekwa sawa kwa Mungu (amina) mpaka mfereji wa Roho Mtakatifu utakuwa mmoja kabisa na Mungu, ni kitu gani kingetukia! Laiti mwanamume huyo na mwanamke huyo wangejiweka sawa, pamoja na uhuru kutoka moyoni mwao, kwa imani kutoka ndani kabisa!

⁴⁸ Watu wengi wanaokuja madhabahuni kuombewa, wana imani ya kiakili. Wao hutubu dhambi zao na kujiunga na kanisa, kwa imani ya kiakili. Wanaamini jambo hilo katika nia ya—yao. Wanaliamini kwa sababu wamelisikia. Wanaamini kwa sababu wanajua ni jambo la busara sana. Lakini hilo silo Mungu analoangalia. Yeye haangalii imani yako ya kiakili.

⁴⁹ Anaangalia moyoni, ambamo humo ndani Mungu... Na wakati linapotoka moyoni, mambo yote yanawezekana wakati huo. Maungamo yako yanakubaliana na maisha yako. Maisha yako yanazungumza kwa sauti kuu kama maungamo yako.

⁵⁰ Lakini wakati maungamo yako yanaposema jambo moja, na maisha yako yanaishi lingine, kuna kasoro mahali fulani. Hiyo ni kwa sababu una imani ya kiakili, wala si imani kutoka moyoni mwako. Na hiyo inaonyesha ya kwamba nje, *hapa*, una maarifa ya Mungu; lakini ndani, *hapa*, kuna pepo anayetilia

shaka. "Ninaamini katika kuponya Kiungu, lakini si kwa ajili yangu." Unaona? "A-ha, ingeweza kuwa, lakini si amini jambo hilo." Umelipata? Nje, unasema "ndio"; ndani, dhamira yako inasema "la." Chombo hicho hicho cha kisayansi kingethibitisha ya kwamba jambo hilo halikuwa sawa, kitalithibitisha.

⁵¹ Angalia wakati wafalme hawa, kabla wao hawajaondoka, walipaswa... Kabla Yehoshafati hajafanya mapatano na Ahabu, alipaswa kusema, "Na tuombe tuone mapenzi ya Mungu ni nini."

⁵² Nipe mhubiri, nipe Mkristo, nipe mke wa nyumbani ambaye ni Mkristo, nipe mkulima, ama mfanya kazi wa kiwanda, ambaye atamweka Mungu kwanza katika kila kitu, nitakuonyesha mtu atakayefanikiwa hata Ibilisi amwekee mambo gani. Yeye humtafuta Mungu, kwanza. Hatuna budi kwanza...

⁵³ Lakini wao hawakufanya jambo hilo. Wote walipofushwa kwa sababu Ahabu alikuwa na ufalme mzuri mkubwa, naye alikuwa amefanya mambo mengi sana, na alikuwa na mambo yake ya ulimbwende, dhahabu zake na fedha, alikuwa mtu mkubwa, aliyefanikiwa, hata hivyo si mwamini.

⁵⁴ Na hapo ndipo ulimwengu ulipo leo. Hapo ndipo Marekani inaposimamia leo. Hapo ndipo makanisa yanaposimamia leo. Tumejenga baadhi ya makanisa makubwa sana yaliyopata kujengwa. Tumekuwa ya wanachuoni stadi sana tuliowahlkuwa nao. Tumefundisha theolojia nzuri sana, na kadhalika, na kujifunza kuimba kama Malaika, lakini hata hivyo kuna udhaifu mahali fulani. Kuna udhaifu, kwa sababu wamefuata fundisho la mwanadamu na roho zinazoshawishi, badala ya kurudi kwenye Neno la Mungu. Wanajaribu kufanya mambo yalingane na ulimwengu. Wamejaribu kuyapamba mambo hayo, kama Hollywood.

⁵⁵ Hapa hivi majuzi, madhehebu yanayoju likana sana, ya makundi ya Full Gospel huko Kansas City, ama, samahani, huko Denver, kwenye mukutano, wanajenga kanisa la dola milioni moja. Na maelfu ya wamishenari wanaongojea senti hamsini kutoka kwa madhehebu yayo hayo, wapate kuipeleka Injili katika nchi za wapagani. Tunachohitaji leo ni ufuluo wa Roho Mtakatifu unaowazia umishenari, uliotumwa na Mungu, utakaokuwa na bidii ya Mungu, kupenya huko ndani katika misitu kule ng'ambo na kumfanyia Mungu kitu, badala ya kujenga makanisa makubwa, mazuri na kujaribu kumshinda jirani.

⁵⁶ Afadhali niabudu kwenye misheni, ambapo pamefagiliwa, ama kwenye mkahawa, na niwe na uhuru wa Roho Mtakatifu na upendo wa Mungu ukichoma miyoni mwetu, kuliko niketi katika kanisa kubwa sana la jimbo tulilo nalo ulimwenguni na nishindiliwe na mafundisho ya mwanadamu na imani za sharti. Tunahitaji leo ufuluo unaotingisha, kurudi kwenye ile Kweli, kurudi kwenye Neno la Mungu tena.

⁵⁷ Sasa, wakati walipotoka kwenda nje, na ilikuwa baada ya kitambo kidogo ambapo Yehoshafati kwa namna fulani alijirudia na kusema, “Je! hakuna... Vema, hebu na tumtake shauri Bwana juu ya jambo hili.”

⁵⁸ Akasema, “Vema,” Ahabu ndiye alifanya hivyo, naye akatuma mtu na kupata mia, wahubiri mia nne waliofunzwa vizuri. Ndipo akawaleta kule na kusema, “Hawa wote ni manabii.”

⁵⁹ Ndipo wakaingia katika kuagua kwao, nao wakaanza kuita. Nao wakasema, “Naam, kwea kwa amani. Bwana yu pamoja nawe.

⁶⁰ Halafu baada ya wote wale mia nne kushuhudia ya kwamba wanapaswa kwenda kwa amani, hata hivyo Yohoshafati akijua... Mnalipata jambo hilo? Mnaona, ndani kabisa katika moyo wa mtu huyo mwenye haki kulikuweko na kitu fulani kilichomwambia kulikuweko na walakini mahali fulani. Kulikuwa na kasoro fulani. Jambo fulani lilikuwa na kasoro.

⁶¹ Ahabu akasema, “Sasa tuna mia nne hapa, na kwa moyo mmoja, kila mmoja wao anasema, ‘Kwea, Bwana yu pamoja nawe’”

Lakini Yehoshafati akasema, “Huna mmoja zaidi?”

⁶² Akasema, “Vema, tunahitaji mmoja zaidi wa nini, baada ya sisi kuwa na watu mia nne watu waliosoma sana nchini? Wote wanasesma, ‘Nenda!’” Hiyo ilikuwa ni kutumia akili. Lakini chini ya moyo wa Yehoshafati alijua kulikuwa na kasoro fulani. Sasa, akasema, “Tuna mmoja zaidi, ye ye ni Mikaya. Lakini namchukia.” Kasema, “Yeye daima anasema jambo fulani baya, akirukia mambo wakati hana shughuli nayo, naye anazamisha makanisa na kila kitu.” Kasema, “Ninamchukia.”

Kasema, “Nenda, kamlete, tuone atasema nini.”

⁶³ Na Mikaya alipokuja, akasema... Wao wakasema, “Sasa, angalia, wewe sema kitu kile kile kama wengine.”

⁶⁴ Akasema, ye ye akasema, “Nitaninii tu...” Hili hapa. Nitasema tu yale asemayo Mungu.” Amina. “Haidhuru nabii wenu anasema nini, na ambayo *huyu* anasema, na ambayo kanisa lako linasema, na yale wasemayo. Mimi nitasema yale asemayo Mungu. Mungu aliyaweka kwenye kinywa changu nami nitasema Yeye asemayo.” Tunachohitaji leo ni Mikaya wengine watakaosema alilosema Mungu. Angalia, kwa hiyo wakampeleka pale naye akasema, “Nipeni usiku wa leo.” Kwa hiyo usiku huo Bwana akakutana naye, naye akarudi asubuhi yake. Wakati hao wafalme wawili walipoketi langoni, akasema, “Kwea.” Kasema, “Kwea. Lakini,” akasema, “Niliwaona Israeli wametawanyika kama kondoo wasio na mchungaji.”

⁶⁵ Kwa hiyo mhubiri huyu mmoja, huku amevaa vizuri kwelikweli, alienda pale akampiga kofi mdomoni, na kusema, “Roho wa Mungu alipita njia gani alipotoka kwangu?”

Kasema, “Utajua utakaporudi.” Naam.

⁶⁶ Akasema, “Sikilizeni hapa!” Akasema, “Sisi ni watumishi wa Mungu. Sisi ni mia nne, nawe ni mmoja.”

⁶⁷ Lakini Mikaya akasema, “Nitawaambia mahali ilipo shida yenu.” Amina! Kasema, “Niliona ono.” Amina! Akasema, “Nami nilimwona Mungu ameketi juu ya Kiti Chake cha Enzi. Niliona jeshi la Mbinguni likimzunguka. Na tunajua ya kwamba Neno la Mungu limetamka laana juu ya mtu huyu, kulingana na yale aliyotenda.”

⁶⁸ Huwezi kubariki kile Mungu alicholaani, wala Ibilisi hawezi kulaani kile Mungu alichobariki. Ni jambo la kibinafsi, haidhuru ni maskini vipi ama ni mjinga vipi, jinsi asivyokuwa na elimu, jinsi asivyo na kisomo. Alichobariki Mungu, kimebarikiwa. Alichalaani Mungu, kimelaaniwa. Jifunze kutofautisha ya kweli na ya uongo.

⁶⁹ Mikaya alijua vizuri kabisa ya kwamba huyo hakuwa ni Bwana aliyeokuwa na hao wahubiri. Vema, wahubiri wale walikuwa na nini? Angalia walilofanya. Walikuwa wamevalia vizuri sana. Walikuwa wamelishwa vizuri sana. Walikuwa wamekusanyika katika karamu zao na kadhalika, na miungano yao, mpaka ikafikia mahali ambapo walijua theolojia zao tu. Na Biblia ilisema ya kwamba Mikaya, wakati alipokuwa anaangalia lile ono, alisema, “Mungu alisema, ‘Tumtume nani ashuke aende kule na kumdanganya Ahabu?’ Ndipo roho wa uongo akasema, ‘Nitashuka niende kule na kumshawishi Ahabu kuititia kwa wale wahubiri, kumfanya Ahabu atoke kwenda kule, kusudi Neno la Mungu lipate kutimia.’”

⁷⁰ Sasa, leo watu wengi sana wanasiliza! (Sasa, shule ya Jumapili, ninapenda hili.) Angalia, watu wengi sana wanasiliza roho zinazoshawishi badala ya kuchukua Neno la Mungu. Roho, ziko ulimwenguni. Ni pepo. Nazo huenda mahali mbalimbali na kuwapagaa watu, wahudumu. Wanawapagaa wafuasi wa kanisa. Wanapagaa watu wazuri. Na kuwafanya waingie katika udanganyifu. Nao wanasema mambo, na kutenda mambo, na kufundisha mambo, na kujizoeza mambo, ambayo ni kinyume cha Neno la Mungu. Leo, wahudumu wa kusanyiko lao wanawaruhusu watu wao kucheza karata kanisani, wengi wao. Sasa, si Wakatoliki kwa jumla, kuna Waprotestanti wengi sana wanaofanya jambo hilo.

⁷¹ Walichojaribu kufanya ni jambo fulani la kibadala. Wamejaribu kukubali mpango fulani mpya. Walijaribu kukubali elimu, kupachukua mahali pa Roho Mtakatifu. Hamtaweza kufanya jambo hilo kamwe, haidhuru mtu wenu ameelimishwa vizuri namna gani. Nafikiri ni jambo zuri kwake kuwa na elimu.

Lakini kama hana Roho Mtakatifu pamoja na hiyo, elimu yake haitamfaa kitu. Elimu haitachukua kamwe mahali pa uongozi wa Roho Mtakatifu. Amina.

⁷² Angalia, wao, badala ya jambo Hili, wamejaribu kukubali kupeana mikono badala ya tukio la kale tulilokuwa tunapata. Leo kanisa limekuwa ni la kisasa. Wao wanaamka na kupeana mkono wa kuume wa ushirika, na hivyo ndivyo karibu jinsi wanavyofanya. Lakini hakutachukua mahali pa kile kiti cha kale cha mwombolezaji ambamo wenye dhambi waliitwa na wakajiweka sawa na Mungu. Hiyo ni kweli.

⁷³ Leo wanajaribu kupachukua mahali pa Mungu pa kutoa zaka. Wanajaribu kukubali jambo fulani. Wanajaribu kulifanya tofauti. Wanashuka kwenda kucheza karata makanisani, wanacheza bahati nasibu. Bahati nasibu kamwe haitachukua mahali pa Mungu pa kutoa zaka. Chakula cha jioni, kuuza mablanketi, pikiniki, kuchangia fedha za kulipia madeni mbalimbali, hakutachukua mahali pa zaka na matoleo ya Milele ya Mungu. Haitapachukua kamwe. Lakini hata hivyo tunajaribu kufanya jambo hilo.

⁷⁴ Ni kitu gani? Ni roho zinazoshawishi zikishuka, zikijaribu kubadi... kubadilisha jambo fulani na Neno la Mungu. Mungu hana kibadala kwa Neno Lake. Ni la Milele na la daima. Mungu hana kitu cha kubadilishana na imani. Imani haina kibadala. Tumaini kamwe halitapachukua mahali pa imani. Imani iko peke yake. Inasimama peke yake. Haitachukua kamwe.... Tumaini kamwe haliwezi kupachukua mahali pake kamwe. Tumaini ni kuwa na hakika ya mambo yatarajiwayo, ni bayana ya mambo yasiyoonekana, ama imani, hasa. Mnaona? Tumaini ni jambo moja; imani ni lingine. Tumaini hutumainia jambo; imani inalo. Moja ni imani ya kiakili; na hiyo nytingine ni ufunuo wa moja kwa moja wa Mungu. Haitapachukua mahali pake kamwe. Tunajaribu, lakini tunatengeneza vibadala hivi vyote.

⁷⁵ Tunajaribu kujenga makanisa makubwa badala ya kuwatuma wamishenari. Kibadala kingine. Yesu kamwe hakumwagiza mtu ye yote kujenga kanisa. Jambo hilo halikuagizwa kamwe katika Biblia. Tumejenga seminari, wameacha jambo hilo kupachukua mahali pa mmishenari. Sisi... Yesu kamwe hakutwambia tujenge seminari. Hizo ni sawa. Elimu, kujaribu kuifanya hiyo ipachukue mahali hapo. Haitapachukua kamwe. Agizo la Yesu lilikuwa “enendemi ulimwenguni mwote mkaihubiri Injili kwa kila kiumbe,” kwa ajili ya wakati wa mwisho. Kwa hiyo vibadala vyote tulivyo navyo havitapachukua mahali pa vitu vya kweli.

⁷⁶ Hivi majuzi nilipata tukio fulani, kibadala. Niliumwa na jino kwa mara ya kwanza, ikanibidi kung’oa jino. Asubuhi ya leo nina jino la bandia linalotokeza hapo ndani. Ninaongea

kwa shida sana. Halitachukua kamwe mahali pa lile halisi. La, bwana! Loo, jamani!

⁷⁷ Unaweza ukamechukua mtu na kumvalisha, umtengeneze kwa mbao, chaki, cho chote utakacho, na kumtengeneza vizuri sana. Hana hisia, hana fahamu. Kamwe hatapachukua mahali pa mtu ye yote halisi. Wala mwongofu bandia anayekuja na kusema, "Nimejiunga na kanisa. Nitajaribu kufanya vizuri zaidi." Hatachukua kamwe mahali halisi pa wongofu wa mtindo wa kale, uliotumwa na Mungu, wa Roho Mtakatifu unaomfanya mwanadamu awe tofauti moyoni. Hauwezi kufanya hivyo, kwa sababu hamna Uzima ndani yake. Hakuna kitu cha kumpa Uzima.

⁷⁸ Hapa si muda mrefu uliopita nilimwona yule mwanasanaa mashuhuri aliyeleta hii, sanamu ya kuchonga, namaanisha, aliyeichonga sanamu hii ya Musa. Siwezi kukumbuka jina lake sasa. Alikuwa ni mwanasanaa wa Kiyunani. Ilimgharimu muda wake wote wa maisha yake. Na wakati alipoifikisha mahali alipofikiri imekuwa kamilifu sana, alifurahishwa sana na hiyo sanamu ya Musa hata akaigonga kwenye goti, na kusema, "Nena, Musa!" Ilionekana ni ya kweli mno! Ilichongwa kikamilifu sana hata ikafanana sana na Musa, kwa mawazo yake, hata akaipiga kwa nyundo ipate kuhisi.

⁷⁹ Inanikumbusha habari za kanisa. Haidhuru utabadilisha kiasi gani, jinsi utakavyopata kusanyiko kubwa, jinsi unavyoimba vizuri nyimbo zako, jinsi kusanyiko lako linavyovalia vizuri, kiasi gani ulivyo na *hiki, kile*, na *kinginecho*, ungaliweza kupiga, kuhisi, cho chote kile. Hakitachukua kamwe mahali pa Uzima, mpaka Kristo atakaposhuka katika mfano wa Roho Mtakatifu, aingie kwenye kanisa hilo, na kulipa tukio jipywa la kuzaliwa mara ya pili. Halitachukua kamwe mahali pa Neno la Mungu. Neno la Mungu linasimama peke yake.

⁸⁰ Mikaya alikuwa na Neno. Alijua alikuwa na Neno. Yeye alikuwa na Neno lililoandikwa, alikuwa pia amelipata Hilo kwa ono. Alijua kile Mungu alichokuwa amesema katika Neno Lake. Alijua yale Mungu aliyosema kwa ono. Yote mawili yalikubaliana pamoja. Alijua ilikuwa ni Kweli, kwa hiyo yeye hakuogopa.

⁸¹ Lakini roho hii inayoshawishi, angalia kile ilichofanya, leo. Kufanya wafuasi wengi wa kanisa, kuwafanya wafuasi bora zaidi wa kanisa, ni imeacha milango wazi katika mafundisho yote ya mtindo wa kale ya Roho Mtakatifu. Iliwaruhusu wanaume kufanya taarifa za kupiga gumzo wao kwa wao, huko kwenye orofa ya chini ambako watacheza michezo. Hilo halitachukua mahali pa kile chumba cha juu, ambapo walikuwa wakiomba kwa ajili ya Roho Mtakatifu. Iliwaruhusu wanawake kukusanyika na kutaniana na kadhalika, na kuwa na upuuzi mwingi usio na maana. Hilo kamwe halitapachukua mahali pa

mkutano wa maombi. Wanawake, vile wanavyotoka na kuva a siku hizi, ni—ni aibu.

⁸² Nilisikia tamshi ambalo Ndugu Neville alitamka, kasema, “Maskini Wamarekani,” kasema, “walipeleka nguo zao zote nchi za ng’ambo.” Hiyo ni kweli. Wanatembea na nguo zao za ndani. Wao... Hiyo ni kweli. Hapana budi walizitoa kwa wamishenari, kwa sababu wamishenari... Hao watu na makafiri katika nchi nyingine wanazivaa. Watu hawa wanakaa bila nguo, inaonekana kama kwamba wanapenda jambo hilo.

⁸³ Nitawaambieni, kuna jambo fulani ambalo limepotoshwa, na hilo ni kuhubiriwa kwa Injili ya Bwana Yesu Kristo. Pepo ndio wanaowavueni nguo. Hakukuweko ila na mtu mmoja katika Biblia aliywahili kurarua nguo alizovaa, huyo alikuwa ni mtu aliyepagawa na pepo. Naye huja katika hali ya upole siku hizi, kana kwamba anawapenda watu, kana kwamba yeze ni mzuri, kama kwamba mambo ni sawa. “Hali ya hewa ni baridi kidogo, na itakufanya uburudike ukipua nguo zako.” Mwanamume akitembea huku na huko uani, nusu uchi, na wanawake vivyo hivyo. Mbona, inafikia mahali ambapo hakuna tena heshima kama ambavyo ingekuwa kwa mbwa, mmoja kwa mwengine. Kuna nini? Sio kwamba ninajaribu kuwaudhi. Ninajaribu tu kuwaambia ni kupagawa na pepo, nanyi mnasikiliza roho zinazoshawishi ambazo zinawaambia, “hilo ni sawa,” lakini ni uongo.

⁸⁴ Punje ya ngano itazaa ngano tu. Kama wewe ni Mkristo, hutafanya jambo hilo. Huwezi kufanya hivyo. Huwezi tu kufanya jambo hilo. Una imani ya kiakili na unasema, “Ndugu Branham, ninaamini Biblia.” Maisha yako yanakuonyesha ya kwamba huamini. Amina. Roho zinazoshawishi zikishindana na Neno la Mungu.

⁸⁵ Yeye alijua mahali alipokuwa anasimama, Mikaya alijua. Yeye alikuwa na Neno la Mungu. Alikuwa ni mtu aliyechukiwa sana. Hakuna mtu aliyempenda kwa sababu yeye alisema Kweli, ingawa wao waliwapenda wahubiri hawa.

⁸⁶ Sasa, jambo lingine lililotukia. Ninaamini na ninafikiri ya kwamba mtu ye yote aliypata kuwa na tukio na Mungu, ama mwanamke, hana budi ajisikie kuchangamka. Ninaamini tu jambo hilo. Hiyo ni kweli. Lakini unajua nini? Wao wamechukua changamko kuwa ni ubatizo wa Roho Mtakatifu. Wao wanapata tu kelele nyingi sana, na hamna kitu humo. Wewe ishi tu kitakatifu tu kama unavyoishi mwenye kupiga makelele, ndipo utakuwa sawa. Michangamko bila shaka ni sawa; “Kujizoeza kupata nguvu za mwili kwafaa kidogo.” Lakini roho zinazoshawishi zimeengia kwenye makundi ya watu wa utakatifu, nao wamewafanya wawe wanategemea tu jambo kwamba eti “kwa sababu wanaweza kupiga makelele”

ama “kwa sababu wanaweza kucheza, kwa sababu wanaweza kuzusha changamko.”

⁸⁷ Yule mzee kule chini, mkuu wa manabii wote, wahubiri, yeeye alikuwa na uhakika sana kwamba alikuwa sahihi, hata akajifanya pembe mbili na kucheza kila mahali, na kufanya kishindo kikubwa zaidi. Yeye alikuwa yuaenda kulisukuma hilo jeshi lingine la Waashuri litoke nchini. Lakini ilikuwa ni uongo! Neno la Mungu lilikuwa limesema tofauti. Amina. Unaona, unaweza ukachangamka kisahihi kama una msukumo wa kweli nyuma ya jambo hilo, changamko la kweli likisababisha kuchangamka kwako.

⁸⁸ Daudi alicheza mbele za Bwana, na mke wake akamcheka. Ndipo Mungu akaangalia chini kutoka Mbinguni, akasema, “Daudi, wewe ni mtu anayeupendeza moyo Wangu.” Lakini nia yake ilikuwa ni sawa. Maisha yake yalikuwa sawa, nyuma yake.

⁸⁹ Kwa hiyo, ati kwa sababu tu tunaweza kuchangamka, haimaanishi ya kwamba tumeokolewa. Kwa sababu tunaenda kanisani, haimaanishi tumeokolewa. Usiziamini hizo roho zinazoshawishi. Roho halisi wa Mungu, Neno halisi la Mungu, ni Kweli ya Mungu; ambayo ni Mbegu ya Mungu, itamzaa Mungu maishani mwako; uwe mcha Mungu, mtauwa, mtakatifu.

⁹⁰ Miongoni mwa watu wengi tunaona mahali ambapo michangamko, na kadhalika, kunakuwako na kupayukapayuka na kusengenyanu, na kila namna ya mambo yasiyo ya kiungu. Ndugu, hiyo ni asidi ya salfuriki kanisani. Ni nguvu za kipepo. Roho za wanaume na wanawake wanazoshirikiana mmoja kwa mwingine, na kujaribu kusukumia mbali, kusema, “Jambo *hili* si sawa, na *hili* si sawa, na *lile* si sawa.” Kama ukilifuatilia, mara tisa kwa kumi ni mtu yuyo huyo anayechochea watu, ambaye hayuko sawa. Amina. Mungu anachukia mafarakano kati ya ndugu. Iweni wenye uchaji, iweni watakatifu, mpendedni Mungu, shikamaneni Naye. Na mradi unajua maisha yako yanaambatana na Biblia, ukiwa mwenye moyo msafi, usafi wa mawazo, upendo kwa ndugu yako, ukijaribu vizuri uwezavyo kuujenga Ufalme wa Mungu, na kufanya mambo hayo, ukivaa inavyopaswa, ukiishi sawa, ukizungumza sawa, ukienda sehemu zinazofaa, ndipo unaweza kuwa na michangamko yote unayotaka kuwa nayo, na kila mtu ataamini jambo hilo.

⁹¹ Yesu alisema, “Ninyi ni chumvi ya dunia. Lakini chumvi ikiwa imepoteza ladha yake, haifai kabisa, ila kutupwa nje na kukanyagwa na watu.” Kama wewe u chumvi peke yake, haifai kitu. Lakini kama una ladha ndani yake, wewe uwe umekolea chumvi na ulimwengu utaona kiu. Kolea chumvi, wao wataona kiu. Loo, jamani!

⁹² Roho zinazoshawishi zikitoka kwenda, pepo ziigizazo. Angalia, tuko katika siku za mwisho. Tuko katika wakati wa mwisho. Ulimwengu uko karibu tayari kufikia upeo wake wa

hatari, kama jipu linalouma sana mahali fulani litakapopasuka moja ya siku hizi na kiini chake kiruke kitoke ndani yake. Umekuwa mchafu. Hakuna dawa inayoweza kuuponya. Wao wamekataa ile—ile chanjo. Wamekataa matibabu. Ukichukua jipu linalovimba pale, na kama hundungwi penisilini ama kitu cha kuliondolea mbali, ama cho chote kile, litaendelea kuvimba tu mpaka lipasuke.

⁹³ Hivyo ndivyo ulimwengu ulivyofanya. Ulianza, si muda mrefu uliopita, kuachilia. Walienda kando juu ya wazo kubwa, pepo wa uongo wakaja na kuanza kuwaambia watu *hivi*, *vile*, ama *vinginevyo*. Tumevunjika-vunjika katika madhehebu mia tisa na kitu, kila moja yakiwa na maoni tofauti. Wanasema, “Tunaamini jambo *hili*, hivi tu! Hivyo ndivyo tu tunavyoamini.” Hawawezi kumruhusu Roho Mtakatifu aingie. Hawawezi kupisha. Mungu akapata kundi la watu ambaeo waliweza kushangilia, basi kila mtu *ilimbidi* kushangilia. Wakawapata wengine ambaeo wangenena kwa lugha, ndipo ikawa kila mtu ni kunena kwa lugha. Wakafanya yote, mpaka ikawa (kitu gani?) kitu kilichopagawa na roho zinazoshawishi kabisa, zikiwashawishi watu kufanya na kuchangamka huku wakati hakuna Mungu ndani ya jambo hilo hata kidogo. Ndipo wanatoka na kuishi maisha yo yote wanayopenda kuishi, na halafu wanaita hicho “ni Ukristo.”

⁹⁴ Nao ulimwengu unaketi na kuangalia, kusema, “Vema, angalia pale! Mimi ni mzuri kama tu walivyo wao.”

⁹⁵ Kama nilivyosema hivi majuzi usiku juu ya nguruwe, kuhusu mwenye dhambi. Huwezi kumlaumu... Mwenye dhambi ni mwenye dhambi. Usijaribu kumgeuza kuwa mwema. Usijaribu kumwambia *hivi*, *vile*, ama *vinginevyo*. Yeye ni mwenye dhambi, kwanza. Yeye ni nguruwe, kwanza. Hajui tofauti yo yote. Kama akienda kwenye sinema, na kuhudhuria Jumapili, na anaenda kwenye michezo ya mpira, na kufanya mambo yote haya, yeye ni mwenye dhambi, kwanza. Asili yake ni kama nguruwe. Maskini nguruwe huingiza pua yake kwenye lundo la samadi na kula nafaka yote humo, na kila kitu; vema, huyo, yeye ni nguruwe. Huwezi kumlaumu. Yeye ni nguruwe. Na hivyo ndivyo ilivyo na wenye dhambi. Lakini unapoenda na kujiita mwenyewe Mkristo, na kuingiza pua yako pamoja naye, basi si bora kuliko alivyo yeye, lakini, wewe ni mbaya zaidi. Tokeni kwake. Achiliensi ulimwengu. Achiliensi. Mruhusuni Mungu. Achilia.

⁹⁶ Unaachilia namna gani? Watu wengi sana wanashangaa leo, wakisema, “Sawa, Ndugu Branham, unaachilia namna gani?” Ninajua mmesikia theolojia kemkem juu ya jambo hilo, “achilia.” Watu wengi wanakazana kutokwa na jasho, wakijaribu kuachilia. Watu wengi huja na kusema, “Nilikuwa naenda kufunga kwa siku arobaini ili niweze kufanya jambo fulani.” Huhitaji kufunga kwa siku arobaini. Unahitaji kuachilia ulimwengu na mambo haya yote ya kipepo, na kuliingiza Neno la

Mungu moyoni mwako. Huna budi kufundishwa jinsi ya kufanya jambo hilo. Hulifanyi kwa kuruka-ruka, wala hulifanya kwa kufunga kwa siku arobaini. Unafanya jambo hilo kwa moyo uliotolewa kwa Mwenyenzi Mungu.

⁹⁷ Kama vile mtoto mchanga. Nilimwona mtoto wangu mchanga kule nyuma, mama yake akijaribu kumvalisha koti lake dogo, asubuhi ya leo. Alikuwa akitaka kuingiza maskini mkono wake mdogo kwenye mkono wa koti. Hakuweza kuingiza mkono wake mle; hajui ataingizaje. Huna budi kuuongoza mkono wake. Anataka kuingiza mkono wake mle, lakini anapapasa papasa kila mahali. Haupati huo mkono wa koti. Yeye anajua hajaingiza mkono.

⁹⁸ Na kwa hiyo unajua ya kwamba wewe huko sawa na Mungu, wakati ungali unasengenya, unasema uongo, unafanya kila kitu. Huwezi kuwa sawa na Mungu, sijali wewe ni mfuasi wa makanisa mangapi, mpaka nafsi yako itakapoongoka. Ndugu, huo ni mtindo wa kale, lakini huo utasafisha kila kitu na kutia supu nafsi ni mwako. Kweli!

⁹⁹ Jaribu kuweka mkono wake ndani, hana budi kuwa na mtu wa kumwongoza, jinsi ya kuingiza mkono wake. Ndipo wakati anapoingiza mkono wake ndani ya koti lake dogo, yeye anajua yuko sawa.

¹⁰⁰ Hivyo ndivyo ilivyo na kila Mkristo aliyezaliwa mara ya pili. Wakati anapoingia kweli katika Mungu, yeye huyachunguza maisha yake na Neno la Mungu na anatambua ya kwamba yeye yuko sawa na kila sehemu Yake. Yeye ana saburi, kiasi, upole, unyenyekevu, nguvu, imani, upendo, furaha, amani. Yeye hasukwisukwi kama bahari yenye mawimbi. Yeye hahofu juu ya kila kitu kidogo. Yeye haruki *hapa na pale*, kama kifuniko cha chupa kwenye bahari yenye upepo mkali. Ametulia. Moyo wake ni msafi. Mawazo yake ni masafi. Nia yake ni safi. Uchaguzi wake ni sawa. Naye anajua analifuata Neno la Mungu. Kuzimu yote haiwezi kumtikisa. Yeye amejiweka sawa na Neno la Mungu. Ana upendo wa Kiungu, usafi wa moyo, kwa kila mwanamume na mwanamke. Yeye ananinii... Yeye ameacha mambo ya ulimwengu, yamekufa kwake; hayataki tena. Mbona, hungeweza kumfanya msichana aliyejazwa na Roho Mtakatifu avaae jozi ya hizo nguo zinazoonekana chafu na kutoka kule nje bila sababu yo yote. La, bwana.

¹⁰¹ Sasa, hakuna haja ya kwenda na kumwambia ya kwamba amekosea, maana yeye hangkuamini, kwa sababu hayo ndiyo yote ajuayo. Hiyo ndiyo furaha yake. Mwanamke anavaa vitu hivyo vidogo, apate kutoka nje jioni, wakati tu waume zao wanaporudi nyumbani, serikali, na kusema, "Wanakata nyasi uani," kwa hiyo... Na mnaniambia jambo hilo ni sawa? Mwanamke, simaanishi kusema wewe ni—wewe ni mwovu. Simaanishi ya kwamba wewe ni mzinzi. Lakini hutambui, ewe

dada, ya kwamba pepo mchafu amekushika. Ungefanya jambo hilo kwa ajili gani? Una akili ya kutosha kujuua ya kwamba si baridi kidogo. Ni joto zaidi. Kuna pepo mchafu.

¹⁰² Unasema, “Ati mimi? Ati mimi, nilienda kanisani!” Nebkadreza alikuwa ni mtu mashuhuri. Lakini, kwa sababu aliingiwa na kiburi, Mungu alimpa roho ya ndama, na akamwacha ale nyasi kwa miaka saba, na makucha yake ya mikono yakakua kama ya baadhi ya hawa wanawake wanavyokua hapa. Hiyo ni kweli. Naye akapagawa na pepo.

¹⁰³ Mtu mmoja alipagawa na pepo na akavua nguo zake. Hawakuweza kumvalisha nguo. Mnaona ninalomaanisha? Ni roho zinazoshawishi.

¹⁰⁴ Kanisa lenu linavumilia jambo hilo. Wahubiri wenu wanaogopa kusema jambo lo lote, wanaogopa ya kwamba hamtalipa zaka zenu tena. Hiyo ndiyo sababu yake. Hiyo ndiyo shida yake. Loo, jamani! Utahubiriaje kundi la koho, isipoikuwa waongoke na wawe sawa na Mungu, kwanza? Wataingiza pua yao katika vitu vilivyokufa wakati wote. Unachohitaji ni kuvitupilia mbali, na kufagia kwa ufufuo wa mtindo wa kale kutoka pwani hata pwani, na kuwafanya wanaume na wanawake kujiweka sawa na Mungu. Achilia, mambo ya ulimwengu! Achilia, yale mahubiri haramu ya kubembeleza. Amina. Hubiri Injili. Mungu alisema hivyo. “Kama ukiipenda dunia au mambo yaliyomo katika dunia, upendo wa Mungu hata haumo ndani yako.”

¹⁰⁵ Watu wanawenza kuruka-ruka, na kushangilia usiku kucha, na kunena kwa lugha kama vile kumimina mbaazi kwenye ngozi ya ng’ombe iliyokauka; watoke moja kwa moja, asubuhi yake, wakiwa na hasira kali sana ya kuweza kupigana na nyati jike, waondoke waende moja kwa moja na kusema jambo fulani kanisani litakalosababisha kanisa zima kuvunjika. Si kitu cho chote ulimwenguni ila roho zinazoshawishi, za kipepo! Mnapaswa kurudi kwenye Neno, ambapo Mungu ni usafi, mtakatifu. Amina. Hiyo ni kweli. Roho zinazoshawishizikishindana na Neno la Mungu!

¹⁰⁶ Huyu hapa mtu, si muda mrefu uliopita, alimchukua maskini mwanamke mmoja... Wakatoliki wana dazani kule. Katika wakati wake wa kupata hedhi, inatokea katika mikono yake na kwenye paji la uso wake. Kama mhubiri mzuri aliye na Roho Mtakatifu... Nilifikiri. Mtu huyo alikuwa na chupa nzima ya takataka hizo, kutoka kwenye mikono ya mwanamke huyo, akienda kila mahali akiwapaka watu kitu hicho. Whiu! Rehema! Ni upinga-Kristo! Sijali kama damu inatoka kutoka kwenye pua yake ama kutoka kwenye kichwa chake, ama wapi, ndugu, hakuna damu itakayopachukua mahali pa Yesu Kristo Mwana wa Mungu. Hiyo ndiyo Damu tu ninayojuua cho chote juu yake. Huenda alikuwa na mafuta yakiniririka kutoka katika mkono

mmoja, na divai kutoka katika huo mwingine, lakini, kama ukiitumia katika aina yo yote ya dini, ni Ibilisi. Kuona jinsi wahubiri watakimbilia upuuzi kama huo!

¹⁰⁷ Tunachohitaji, ni kurudi kwenye Kitabu cha Mwongozo, kurudi kwenye Neno la Mungu! Hili ndilo Neno la Mungu, Biblia ya kale iliyobarikiwa. Unasema, "Vema, ninahofu kuwa kitu hicho, Ndugu Branham. Ninahofu nitapoteza kiasi fulani cha furaha yangu." Kuna nini? Hujui furaha ni nini.

¹⁰⁸ Nimesema simhukumu mnywaji pombe kwa kutoka kwenda na kulewa. Yeye amejaa huzuni. Hajui. Anaamka, asubuhi moja, yeye ana moyo wa huzuni, ana kizunguzungu cha pombe. Anaondoka anaenda anajipatia chupa mbili tatu za bia, na anaondoka na kununua wiski, na upuuzi wote wa namna hiyo.

Maskini huyo mvuta sigara anaketi kitako na kuvuta sigara, na kupulizia kwenye pua yake kana kwamba alikuwa gari moshi la mizigo. Hivyo tu. Mimi simlaumu; hiyo ndiyo furaha yote aijuayo. Hivyo ndivyo tu ajuavyo. Yeye ni nguruwe, kwa tabia yake.

¹⁰⁹ Hamna aibu ninyi mnaodai kuwa Wakristo na kutegemea vitu kama hivyo mpate furaha, wakati Injili ya Roho Mtakatifu si kitu ila nyumba moja kuu mno ya kutoa nguvu za shangwe. Injili ya Roho Mtakatifu ni kileo kikamilifu cha kila mtu mwenye moyo mzito. Utakunywa kinywaji cha Yesu Kristo, ujazwe na Roho Mtakatifu, umelewa mpaka utakapoondoka katika ulimwengu huu, amina, furaha isiyotamkika na ilijojaa utukufu. Kuna uchangamfu daima. Ni kiburudisho cha daima, umelewa mchana na usiku! Amina. Hilo ni Neno la Mungu.

¹¹⁰ Kanisa linakuja, linakubaliana na mambo mengine. Hawana budi kuwa na karamu kidogo ambapo wote wanaenda kwenye ukingo wa bahari, kwa mapumziko. Karamu ya kadi pamoja, kwa ajili ya ushirika. Hiyo ni kweli. Wanacheza dansi, mara kwa mara, katika nyumba ya mfuasi mmoja, mara kwa mara katika sebule ya kanisa. Dansi, wakiiruhusu, wakijaribu kupata jambo fulani la kuwatoshaleza. Kuna nini? Wao ni kundi kubwa la nguruwe, hata hivyo. Wao ni nguruwe, kwanza. Kama watakutana na Kristo kamwe, wangekuwa na furaha nyingi sana, mambo hayo yangetkuwa mafu kuliko usiku wa manane, kwoo. Injili, kulewa katika Roho, furaha isiyotamkika na ilijojaa utukufu!

¹¹¹ Usimlaumu mwenye dhambi; mhurumie. Acha aondoke aende avute kiko chake, acha anywe pombe yake, acha afanye karamu yake ya yadi. Hiyo ndiyo furaha yake. Usimlaumu. Akija nyumbani na kila kitu, amechoka na kudhoofika, anataka kiburudisho fulani. Jambo la wewe kufanya ni kuishi maisha ya kitaua hivi kwamba unawenza kumthibitishia ya kwamba Injili ina mara elfu kumi ya mambo hayo, kwake. [Mahali patupu kwenye kanda—Mh.] Na kama akifa katika hali hiyo, ataenda

kuzimu, na pombe zake. Huo ni ulevi wa Ibilisi. Kama akifa, akikokota kiko hicho cha kale, Mungu ndiye hakimu wake. Kama akifa, akitoka huko nje, akicheza dansi, na kuzurura amevaa nguo za kizinzi, Mungu ndiye Hakimu wao.

¹¹² Lakini kuna jambo moja, kama ukifa chini ya Nguvu za kutia mafuta za Roho Mtakatifu, kama alivyofanya Stefano alipouangalia uso wa Mungu, kasema, “Ninaona Mbingu zimefunguka, na Yesu amesimama katika mkono wa kuume wa Mungu,” wewe unealekeea Mbinguni, kama vile mbayuwayu kwenye kiota chake. Amina.

¹¹³ Roho zinazoshawishi dhidi ya Neno la Mungu! Achilia, achilia. “Unafanyaje jambo hilo, Ndugu Branham?” Achilia tu. Hivyo tu ndivyo inavyokupasa kufanya. Lichukue Neno la Mungu. Usijaribu kubuni cho chote. Usipige magoti madhabahuni na kuyapigapiga, na kulia, “Mungu, nipe Roho Mtakatifu! Bwana, nipe Roho Mtakatifu!” Yeye haji, kwa wewe kupigapiga madhababu hiyo. Hilo halifai kitu. La. Hivyo sivyo anavyokuja. Ni, kuamini Neno Lake!

¹¹⁴ Mwangalie Petro. Petro alikuwa katika shida, ilionekana kana kwamba atakufa. Naye akamwona Bwana akija, anatembea juu ya maji. Ndipo akasema, “Bwana, ikiwa ni Wewe, niamuru nije.”

Bwana akasema, “Njoo.”

¹¹⁵ Sasa Petro akasema, “Sasa ngoja kidogo, Bwana, naomba nifunge kwa siku arobaini, nione kama ninaweza kwenda juu ya maji hayo, ama siwezi. Ee Bwana, naomba nipate Roho wa Kutosha juu yangu, nipate kucheza katika Roho na kunena kwa lugha, katika mtumbwi huu, ndipo ninaweza kutoka nje”? La, bwana! Yeye aliamini Neno la Mungu, akaachilia na kuacha. Mungu akamfanikisha.

¹¹⁶ Vipi kama Mungu alikutana na Musa, na kusema, “Musa, shuka uende Misri, ukamwambie Farao, ‘Waachilie watu Wangu waende’”? Vipi kama Musa alisema, “Naomba nifunge siku arobaini, kwanza, nione kama nina nguvu za kutosha kukutii Wewe, Mungu. Nipe kitu fulani, kitu fulani, Bwana. Hebu nikwambie jambo fulani, hebu nione kama ninaingia katika Roho, kwanza”? Musa hakuuliza maswali, aliamini Neno la Mungu, akaenda zake. Hivyo ndivyo unavyopaswa kufanya, kuamini Neno la Mungu. Ndipo utajua utawenza kufanya jambo hilo. Yeye hakungoja mpaka jambo lingine likatukia, yeze alienda moja kwa moja akafanya hivyo.

¹¹⁷ Vipi kuhusu Eliya, wakati aliposhuka kutoka Mlima Karmeli, alikuwa amekaa kule muda mrefu? Ndipo akakutana na mjane maskini. Alikuwa... Alikuwa mgeni, Mtaifa. Na wakati alipokutana naye kule chini, alikuwa anaokota kuni uani. Ndipo Mungu akamwambia, “Shuka uende kule katika nyumba ya yule mjane.” Ni mahali pa jinsi gani kwa mhubiri kwenda!

¹¹⁸ Ndipo anashuka anaenda kwa nyumba ya yule mjane. Naye alipofanya hivyo, alikuwa na kuni mbili. Kasema, “Unafanya nini?”

¹¹⁹ Kasema, “Ninaokota kuni. Nina unga wa kutosha tu kuoka keki chache za unga wa mahindi. Huo tu ndio uliosalia. Ni miaka mitatu tangu tulipopata mvua.” Ndipo kasema, “Basi nitaoka hizi keki za unga wa mahindi. Nami pamoja na mvulana wangu tutazila, kisha tufe.”

¹²⁰ Yeye akasema, “Niokee moja, kwanza!” Haleluya! Loo, ninajua mimi nina kichaa kidogo, lakini niko upande wa Bwana, hata hivyo. Kasema, “Niokee moja, kwanza. Kwa kuwa, BWANA ASEMA HIVI.” Unaona basi.

¹²¹ Ni kitu gani? “Utafuteni kwanza Ufalme wa Mungu, na haki Yake.” Si Ufalme wa Mungu na “kelele kidogo,” si Ufalme wa Mungu na “mwamsho mdogo,” si Ufalme wa Mungu na “*hili* na *lile* kidogo.” Lakini, “Mungu, na haki Yake, na mambo haya mengine yote mtazidishiwa.” Weka kwanza!

¹²² Sasa, mjane huyo alisikia jambo hilo. “Imani chanzo chake ni kusikia, kusikia Neno.” Akasema, “Hilo ni Neno la Bwana, kwa kuwa huyo ni mtu mtakatifu wa Mungu. Huyo ni nabii wa Mungu, nami ninajua ni kweli. Na hilo ni Neno la Mungu.”

¹²³ Sasa, yeye hakukimbia kule kuwaliza majirani jinsi ya kufanya jambo hilo. Yeye hakutaka kwenda kushiriki ninii yake...na kuwaambia majirani, kusema, “Sasa, mnaonaje? Yule mhubiri yuko nyumbani mwangu, akisema jambo *hili*. Susie, unaonaje juu ya jambo *hili*?

¹²⁴ Akaingia, akaanza kutoa nje. Akaachilia. Akaachilia aliyokuwa nayo, kusudi apate zaidi. Hilo ndilo ulimwengu unahitaji leo, ni kuachilia uliyo nayo ya mtindo wa kale. Haleluya! Alitupa nje, kusudi apate kujazwa. Alitupa mafuta yote aliyokuwa nayo, na mafuta yote aliyokuwa nayo na unga wote aliokuwa nao, kwa mhubiri huyo, kwenye Ufalme wa Mungu. Na wakati alipotupa yote mle ndani, Mungu akashuka, akajaza lile pipa, akajaza ule mdumu wa mafuta. Akatupa tena, kwenye sahani ya yule mhubiri. Nayo ikarudi, imejazwa tena. Akatupa ndani. Kila alipotupa, Yeye alijaza.

¹²⁵ Nitasema, leo, kama mtu atatupilia mbali upuuzi huu wote wa kufanya yasiyofaa, na kuiga Ukristo, na kumruhusu Roho Mtakatifu kupachukua mahali Pake, kutakuweko na ufufuo utakaoanza kwenye barabara ya Nane na ya Penn ambao utaenea nchini mwote. Acheni upuuzi. Rudini kwenye Neno la Mungu. Tupeni nje, mpate kujaza. Achilieni, Naye Mungu ataacha aje. Wewe tupa nje, Mungu atajaza. Mambo yote madogo-madogo, ya, “Huna budi kufanya jambo *hili*, na huna budi kufanya jambo *lile*; na unapaswa kufanya *hivi* na unapaswa kufanya *vile*.” Sahau! Yatupe nje ya nafsi yako!

¹²⁶ Sema, “Mungu, nijalie mimi, tangu ninii kabisa...siku ya leo, niwe Wako kabisa. Bwana, naja kwa moyo uliovunjika. Ninakuja kwa roho iliyio ya toba. Ninakupenda. Unajua ninakupenda. Nami ninataka kusahau upuuizi huu wote wa siku hizi zote arobaini za kufunga na nione kama ninaweza kumkaribia Mungu, na yote *haya, yale, yale mengine*, upuuizi huu wote.”

¹²⁷ Acheni jambo hilo! Hakuna kitu ndani ya Neno kinachokwambia ufunge siku arobaini. Hakuna hata kimoja. Hakuna kitu ulimwenguni kinachokwambia ufunge, isipokuwa Mungu akwambie. Ukipunga, hutapata njaa, na kufanya mambo haya yote. Unapofunga, ndugu, utakuwa na shangwe na furaha wakati wote. Kasema, “Msionekane mbele za watu kama wanafiki wanavyofanya, wakiwa na nyuso ndefu, na uso wenye huzuni. ‘Mimi niko kwenye mfungo wa siku arobaini, nguo zangu hazitanitosha tena. Nimepoteza ratili thelathini, na watu waliniambia nitaonekana mzuri baada ya jambo hili kwisha.’” Loo, upuuizi! Ni roho zinazoshawishi za Iblisi.

¹²⁸ Unapanda unaenda madhebahuni, na kusema, “Utukufu, utukufu, utukufu” mpaka huwezi kusema jambo jingine lo lote, na kusema, “Huna budi kunena kwa lugha kabla hujampokea Roho Mtakatifu.” Upuuizi! Tupilia mbali!

¹²⁹ Ondoa jambo hilo ndani yako na uje kwa Neno la Mungu! Akasema, “Tubuni, kila mmoja wenu, mkabatizwe katika Jina Lake Yesu Kristo kwa ondoleo la dhambi zenu, nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu.” Ikiwa Mungu hatimizi Neno Lake, Yeye si Mungu. Amina. Tupa nje. Jazwa. Amina. Whiu! Ninapenda jambo hilo. Hilo ni Neno Lake. Mungu alisema jambo hilo. Hiyo ni kweli. Na hapo Mungu aliposema jambo hilo, Mungu atalishughulikia. Vema. Matayarisho yote unayofanya, kwenda kote kanisani unakoenda... .

¹³⁰ Ni kama tu hapa chini kwenye kiwanda cha motokaa mahali walipotengeneza mabehewa makubwa, ama kundi la mabehewa ya abiria. Nilikuwa ninafanya kazi mle. Nao wanachukua na kutengeneza mabehewa hayo makubwa na, na kuweka mbao ngumu, zilizozungushiwa mpingo, na kila kitu vizuri sana, wanayaweka kule nje kwenye reli, nayo ni mafu kama msunari wa mlango. Hiyo hapo injini, hamna mvuke ndani yake. Iko pale tu.

¹³¹ Inachohitaji leo ni moto kwenye boila. Inachohitaji leo ni mvuke kidogo. Inachohitaji leo, kanisa, kuchemsha; kitu kilicho na joto sana kinachochemshwa kule ni kuchemsha dhambi kutoka katika maisha yako, ni upendo. Na kama hamwezi kupendana ninyi kwa ninyi, mtampendaje Mungu Ambaye hamjamwona? Upendo huficha dhambi nyingi. Mpendeni Mungu, ndipo mtapendana ninyi kwa ninyi, ndipo mtalipenda

kanisa, mtaipenda Huduma hii, mtapenda kila kitu kilicho cha kitauwa, nanyi hamtayakaribia mambo ya ulimwengu.

¹³² Roho zinazoshawishi zikienda kila mahali zikiwaambia watu *hiki, kile*, ama *kinginecho*, “Wao hawana budi kufanya *hivi*. Hawana budi kufanya *vile*.” Ni kwa sababu madhehebu yameinuka, nao wana ufunuo mdogo ambapo wanasema, “Vema, sasa, ninaamini ya kwamba mtu... Ninaamini katika kitu kama kupaza sauti katika Biblia.” Hiyo ni kweli. Huo ni ukweli. Wao waliunda madhehebu kutokana na jambo hilo, “Wakati unapopaza sauti, unaye.” Bali huna.

¹³³ Wengine wakasimama, kasema, “Ni kunena kwa lugha.” Hilo ni kweli. Hilo liko katika Biblia. “Vema, hapo unaponena kwa lugha, unaye.” Lakini wengi wao walinenya kwa lugha wala hawakuwa Nay. Mnaona? Sivyo ilivyo. La, bwana.

Wengi wao walisema, “Vema hatuna budi kutoa unabii.”

¹³⁴ Waangalie manabii hawa hapa wakiwa na pembe kichwani mwao, wakirukaruka na kutoa unabii. Mikaya akasema, “Ninyi, kila mmoja wenu, anasema uongo.” Amina. Sawa. Mungu haji namna hiyo. Mungu huujia moyo mnyenyeketu unaoambatana na roho ya toba, iliyovunjika. “Yeye aendaye zake, akipanda mbegu kwa machozi, bila shaka atarudi tena akifurahi, akileta miganda ya thamani.” Amina. Pata jambo hilo vizuri, ewe rafiki.

¹³⁵ Elimu nyingi sana juu ya pepo, pepo wakitenda kazi katika nafsi za binadamu! Angalia mahali hilo linapozalia tunda lake. Angalia kwamba mtu huyo anaishi maisha ya aina gani. Angalia jinsi wanavyoishi, angalia jinsi wanavyofanya, angalia nia yao ni nini. Haiwezekani tu... Na kama niliwaambia ya kwamba, “Njia pekee... Haya hapa magari, yote yajipanga kwenye mstari hapa. Mbinguni ni Charlestown. Huwezi kwenda kwa miguu. Njia pekee unayoweza kuendea, ni kwa gari. Na kila mtu anayevuka mstari huo hana budi kuleta galani tano za mafuta.” Hili hapa gari lake, lakini kama hana petroli hawezи kuliendesha. Vema, hivyo ndivyo ilivyo hasa, kabisa Mbinguni. Kama ukifa bila Mungu, sijali jinsi unavyoishi na uliunda magari mangapi, kama upendo wa Mungu hauko mle kukuvuta uingie katika Ufalme wa Mungu, umepotea.

¹³⁶ Kuna negativu na positivu. Haidhuru ni kiasi gani cha umeme huu kinapita hapa, kama hauna waya wa ardhi, hautatoo mwangaza. Hiyo ni kweli. Huna budi kuwa imara, umetiwa msingi katika upendo wa Mungu. Loo, ndugu! Leta hiyo negativu na positivu pamoja, utapata Nuru, ile Nuru ya mtindo wa kale ya Injili. Acha imulike pwani hata pwani. Hutaipata kamwe bila Hiyo. Haidhuru unaweza kujitikisa namna gani na kuruka-ruka kwa positivu, huna budi kuwa na waya ya ardhini kuwashaa mwanga. Amina.

¹³⁷ Je! uliwahi kutambua? Unaweka waya wa ardhini hapa kwenye hii, ukiweka waya wa ardhini hapa kwenye hii, kila kitu

kitarudi hapa chini kwenye kituo kidogo, papa hapa ardhini. Na kila mara mtu anapoimariswa na kuwékwa msingi katika Neno la Mungu, linamwimariswa na kumweka msingi Kalvari, huko ng'ambo, ambapo nanga, ile nguzo ya kushikiza ya Mungu ililetwa kule, kuwasha Nuru ya Injili. Amina.

¹³⁸ Unajua shida ni nini? Watu kwenye nyumba hizi kubwa baridi za kuwekea maiti hapa nje, zinazojifanya kwamba zinahubiri Injili. Maskini mhubiri mdogo alinijia jana, yeche nje ni mshiriki wa madhehebu yaliyo makuu sana yaliyopo nchini, nje ya Katoliki. Yeye alisema, "Ndugu Branham, nimechefuliwa moyo na nimechoka." Kasema, "Watatufanya sisi wahubiri wote kuva majoho na ukosi uliopinduliwa, na—na kuhubiri mambo fulani. Nao watatwambia tuhubiri nini, kila baada ya miezi mitatu." Akasema, "Siwezi kuvumilia jambo hilo tena." Akasema, "Nifanye nini? Inanibidi nianze kuihubiri Injili?"

¹³⁹ Nikasema, "Ndugu, mradi tu uko pamoja na madhehebu hiyo, iheshimu. Sema tu yale wanapaswa kusema. Lakini mwendee mzee wako wa kanisa ama kiongozi wa jimbo, na kumwambia, 'Bwana, nimezaliwa mara ya pili kwa Roho wa Mungu. Hili hapa Neno la Mungu. Kama utaniruhusu kuhubiri Hilo, nitakaa kanisani mwako. Kama huniruhusu, nitaondoka. Utampa mtu mwingle." Hiyo ndiyo njia ya kufanya jambo hilo. Ussitesite. Usiwakanushe. Jitokeze useme jinsi mambo yalivyo. Vema.

¹⁴⁰ Akasema, "Ndugu Branham, unafikiri ningekuwa na kusanyiko?"

¹⁴¹ Nikasema, "Palipo na mzogo, ndipo wanapokusanyika Tai." Hiyo ni kweli, watafuata.

¹⁴² Kama yule mtu, siku moja, aliywaaangua kuku. Sasa, si mzaha. Simaanishi hilo kama mzaha. Ninasema jambo muhimu. Alikuwa anataka kuku wake waatamie, naye hakuwa na mayai ya kutosha. Akaweka yai la bata chini ya mmoja. Na wakati yote yalipoanguliwa, yule bata alikuwa ndicho kitu cha kuchekesha sana walichowahi kuona hao kuku. Kwa hiyo wakati kuku angeita hao vitaranga na hivyo vifaranga vingejuja, lakini yule bata hakujuu lugha hiyo. Lakini, siku moja, maskini yule kuku wa kale akawaongoza nyuma ya ghala ya nafaka. Kulikuweko na ghuba ndogo nyuma ya kile kitaku. Wakati maskini bata huyo mdogo alipopata harufu ya maji, aliyakimbilia hayo maji upesi alivyoweza. Maskini yule mama kuku wa kale akasema, "Kluk, kluk, kluk." Naye yule bata mdogo akasema, "honki, honki, honki." Alikuwa anaelekea majini. Kwa nini? Yeye alikuwa bata, asili yake. Alipoyanusia maji, ndugu, hakuweza kuyaacha, kwa maana yeche alikuwa ni bata.

¹⁴³ Nami nasema leo, watu wo wote wanaotaka kumwona Mungu kweli, hawataliruhusu kanisa lo lote liwaamrie mambo hawawezi kuishi, *haya* ama *yale*. Ikiwa una tabia ya Mungu

ndani yako, utaendea utakatifu. Utaliendea jambo lililo sahihi. Utasimamia jambo lililo sahihi. Utafanya jambo lililo sahihi. Utawazia jambo lililo sahihi. Utaishia jambo lililo sahihi. Ikiwa wewe ni bata, utayapenda maji. Ikiwa wewe ni Mkristo, utampenda Kristo. Ikiwa wewe ni ibilisi, utayapenda mambo ya Ibilisi. Ikiwa wewe ni koho, utakula vitu vilivyokufa. Ikiwa wewe ni nguruwe, utakula samadi. Uko wapi leo? Vema. Wewe unayedai uko hapa juu, ukila vitu vya Bwana, kisha unashuka unaenda na kushirikiana na Iblisi? Jambo hilo lina kasoro. Acha kuwasikiliza hao roho; hao ni pepo. Haidhuru kama itakubidi kusimama peke yako. Wanaume na wanawake amba wamewahi kuwa jambo lo lote, karibu wote, wamekuwa ni wanaume na wanawake waliosimama peke yao na Mungu.

¹⁴⁴ Mwangalie Mikaya, jinsi alivyosimama pale; si kama ule mwamba wa Gibraltar, bali kama Mwamba wenyi imara. Yeye alisema, “Sitasema kitu... Sijali seminari zinasema nini. Sijali kusanyiko langu linasema nini. Sijali mfalme anasema nini. Kama wakinikata kichwa, nitasema tu yale Mungu anayoweka kinywani mwangu kusema.” Yeye alikuwa sahihi. Alikuwa sahihi.

¹⁴⁵ Na siku hizi, wanaume na wanawake, hawajali yale ulimwengu uliyo nayo kwa ajili yako, ushawishi ulio nao, wana mchanjo wa bakteria zipi walio nao, na kudai, “Ukijiunga na kanisa, utakuwa sawa.” Huo ni mchanjo wa uongo. Kwa nini? Ungali una huo ugonjwa wa dhambi. Hiyo ni kweli. Lakini ninakwambia kitu kimoja, ndugu, kitakachokuchanja kutokana na dhambi, hicho ni, njoo kwenye Damu ya dhamani ya Bwana Yesu Kristo na ujazwe na Roho Mtakatifu, na jambo hilo litakuchanja kutoka katika dhambi yote, na shauku zako zitaelekezwa Mbinguni, wala hutakuwa na wakati wa mambo ya ulimwengu.

Na tuombe.

¹⁴⁶ Baba yetu wa Mbinguni, tunaziona hizi roho zinazoshawishi juu ya watu, na tukijua ya kwamba zinayadharau mambo ya Mungu, ninaomba, Mungu, ya kwamba utamshika kila mwanamume na mwanamke aliye hapa ndani leo. Hebu huyu awe bibi, Bwana, atakayetambua ya kwamba maisha yao hayaambatani na Neno. Na wamekuwa wakisikiliza jambo mbaya, ambapo ibilisi amekuwa akiwafariji kwa magazeti ya Hadithi ya Kweli, upuuzi ulioza wa ulimwengu, na sinema zilizooza na televisheni chafu. Ee Mungu, ni mambo yasiyowezekana kabisa kwa Mkristo kuangalia! Mungu, linatuchukiza. Ulisema lilikuchefua moyo, kama matapiko. Ulisema, “Mbwa huyarudia matapiko yake, na—na nguruwe kwenye matope yake.” Maskini mbwa atatapika kitu fulani. Unamwona maskini mtu aliyezaliwa nusu, anavyodhaniwa amezaliwa, huyo mnafiki atakuja madhabahuni, na inaonekana kana kwamba utautapika ulimwengu; wanaendelea tu,

wanarudi moja kwa moja na kula kitu hicho tena. Ee Mungu, isafishe Nyumba Yako, Bwana. Haleluya! Mtume Roho Mtakatifu akiwa na sadikisho kubwa sana la makosa ambaye atasafisha shauku za mtu na kuisafisha nafsi yake, na kumsafisha kabisa na kumfanya kiumbe kinachoelekeea Mbinguni. Mpe ye... Ufanye upya ujana wake na nadhiri zake kama tai, apate kuruka na kupita mambo ya ulimwengu huu, na kupanda aingie huko Mbinguni ambako anawenza kuona shinda zikija kwa mbali. Tujalie, Bwana.

¹⁴⁷ Uliwalinganisha manabii Wako nao, na tai, ya kwamba walikuwa na jicho la tai, wangeweza kupaa juu sana na kuona mambo mapema sana kabla hayajatukia. Ee Mungu, libariki kanisa hili dogo. Wabariki watu wanaokuja hapa. Wabariki wageni malangoni leo. Na jalia wajue ya kwamba Ujumbe huu haukuelekezwa kwa mtu binafsi, lakini ulielekezwa hasa, Bwana, kwa hao walio na haja sana; tukijua ya kwamba siku moja hatuna budi kusimamam katika hukumu ya Mungu, na tukijua ya kwamba tutawajibishwa kwa kujua ile Kweli na kuitangaza. Baba, naomba ya kwamba litachukuliwa na kila moyo. Katika Jina la Yesu.

¹⁴⁸ Huku vichwa vyetu vimeinamishwa kidogo, sijui kama kuna mtu fulani hapa asubuhi ya leo ambaye angesema, “Ndugu Branham, nimechefushwa moyo na kuchoshwa na mambo haya madogo yaliyooza. Nina mambo madogomadogo ambayo yamenilemea kwa muda mrefu sana. Daima ni—ninazungumza mahali nisipopaswa kuzungumza. Ni—ninafanya mambo nisiyopaswa kufanya, na ninajua jambo hilo. Si jambo zuri kwa Mkristo. Sitaki kufanya jambo hilo; Mungu anajua sitaki. Wala sitaki kumsikiliza roho huyo wa kale tena. Hilo ndilo jambo ambalo limenizua maishani mwangu mwote, kuwa upendo halisi na uhuru katika Kristo. Nataka uniombee, Ndugu Branham, ya kwamba lita— litaondoka leo. Waweza kuinua mkono wako? Kila kichwa kiinamishwe. Mungu awabariki. Loo, jamani, mikono dazani kadha! Mambo madogomadogo ya kale yasiyo na faida, mambo madogo ya kale yanayokufanya uzungumze ama kuanza mzozano mdogo kanisani, yanayokufanya uunge mkono jambo moja ama lingine. Loo, hiyo ni kutokuwa mtauwa. Hayo ni mafarakano kati ya ndugu. Na usifanye jambo hilo. Hutaki jambo hilo. Hutaki mambo hayo madogo ya kale, hasira ndogo na cho chote kile, kukushusha moyo.

¹⁴⁹ Sema, “Mungu, sitaki kitu hicho tena. Kimenichefusha moyo na kunichosha. Niko tayari leo kukitupa. Ninakuja sasa, Bwana, nami ninataka kuacha uchoyo wangu wote. Kama ndugu yangu hanitendi mema, nitamwombea hata hivyo. Kama baba yangu hatanitendea mema, nitampenda hata hivyo. Kama mke wangu hatanitendea mema, ama mume wangu, nitatembea, nikiwa mnyenyeketu, mbele za Mungu. Bwana, ninautazama tu Ufalme

Wako. Ninataka nia yangu inyoke. Ninataka moyo wangu ujae furaha. Ninataka kutembea, wakati shida kweli zinapovuma karibu nami, bado ninataka kukaa nimeinua mikono yangu na moyo wangu ukiwa msafi mbele Zako, Bwana, nikijua jambo hili, ya kwamba siku moja nitakutana Nawe. Ninataka tukio la namna hiyo. Bwana, nifanye jambo hilo, tangu sasa.”

¹⁵⁰ Unaweza kuinua mkono wako, mtu fulani ambaye hakuinua mkono wake muda kidogo uliopita. Mungu akubariki. Mungu akubariki. Dada, tupe sauti ndogo wakati tumeinamisha vichwa vyetu. Unamaanisha jambo hilo kiasi gani kwa kweli? Usicheze sasa. Huu sio wakati wa kucheza. Huu ni wakati wa kupokea. Huu ndio wakati unaopaswa kupata jambo Hilo. Njoo, kitupilia mbali sasa hivi. Utafanya hivyo? Njoo, mtollee Mungu yote uliyo nayo. Useme, “Mungu, sina mengi sana. Mimi ni maskini mke wa nyumbani tu. Siwezi kufanya mengi, Bwana, lakini ni—ninaweza kusoma Biblia Yako, ninaweza kuomba kila siku. Ninaweza kutupilia mbali uchafu wote ulio katika nia yangu. Ninaweza kutupilia mbali upuuzi huo wote. Nina hatia ya mambo mengi sana ambayo yule mhubiri alisema asubuhi ya leo, kwa hiyo ni—ninayatupa nje leo. Siyataki. Mungu, nijaze kwa upendo. Nijaze na kitu kinachonifanya nimpende adui wangu aliye mbaya sana. Ninakitaka kweli, Bwana.”

¹⁵¹ Wakati anapoomba hapa, mbona usije sasa na kusimama madhababuni kidogo tu, wakati tunapokusanyika katika maombi. Kama kweli unamaanisha jambo hilo sasa, kama kweli wewe uko tayari kuacha mambo hayo, hutaacha madhababu haya leo ukiwa na hayo moyoni mwako, kama utakuja kwa unyenyekevu. Na kusema, “Ninakuja hapa kusimama tu, kwa muda kidogo, Ndugu Branham, naam, wakati unapoomba pamoja nami, mimi binafsi.” Na— nawatakeni mje, mkaombe. Utakuja sasa? Huku vichwa vyenu vimeinamishwa, ni nani atakayesimama na kuja madhababuni, asimame karibu na madhababu?

Usinipite Mwokozi,
Unisikie;
Unapozuru wengine,
Usinipite.

Yesu, Yesu,
Unisikie;
Unapozuru wengine,
Usinipite.

¹⁵² Haidhuru umekuwa Mkristo kwa muda mrefu kiasi gani, na ungali una hizo roho za kale zinazozungumza nawe, zinakufanya ushikwe na hamaki, zinakufanya kumsengenya mtu fulani. Wakati mtu fulani anapokuja na kuanza kumsengenya mtu mwingine, unaungana moja kwa moja nao, loo, unawararua tu. Hilo ni kosa, ndugu. Usifanye hivyo. Hilo hatimaye litakuzuia

kuingia katika ile Nchi ya Ahadi. Kama una mambo madogo ya miaka mingi ambayo hupaswi kuwa nayo, kama upendo wa Mungu kweli haumo moyoni mwako, si uwe bibi na mwanamumee kwelikweli, uje hapa na kusema, “Mungu, nitayatupa papa hapa, asubuhi ya leo, papa hapa. Nitaondoka hapa madhabahuni nikiwa mtu tofauti.” Si uje?

¹⁵³ Kuna mwenye dhambi ye yote ambaye hajamkubali Yesu, nawe unajua wewe ni mwenye dhambi, humjui kama Mwokozi wako? Sema, “Ndugu Branham, naam, nadhani nilikuwa na anasa nyingi sana. Ninaenda kwenye madansi na kwenye mambo yote hayo. Ninaangalia picha mbaya za sinema. Na ni—ninasoma vitabu vibaya. Ninasoma vitabu vya kale vilivyo na hadithi chafu. Kwa namna fulani ninafurahia kuvisoma.” Ndugu, una kasoro. Hiyo ndiyo ladha yako; unaona, acha nione anayosoma mtu, hebu nione anayoangalia, nisikilize muziki anaosikiliza.

¹⁵⁴ Hivi majuzi, nilipokuwa nikija kwa gari fulani, mtu fulani alinyosha mkono akafungulia redio yangu, namna fulani ya muziki mchafu. Nikasema, “Ifunge hiyo. Sitaki kusikia huo.” Namna fulani ya nyimbo chafu.

Akasema, “Mbona, ninapenda kuusikiliza.”

Nikasema, “Tabia yako ni baya. Umekosea.”

¹⁵⁵ Nilipokuwa huku nje, siku chache baada ya jambo hilo, huko juu kando ya mlima ama ya kilima, nikivua samaki, pamoja na mtu huyo. Hao ndege wadogo walikuwa wanaimba. Kipozamataza walikuwa wanapiga makelele ya furaha. Yule mbayuwanyu wa kale alikuwa anaruka hewani, ama kirukanjia, akiimba sifa. Nikampigia makelele yule mvulana, nikasema, “Angalia, jamani, huo ndio muziki wangu. Ifungulie hiyo. Hiyo ndiyo redio yangu. Mungu huwatuma waniimbie ninapokuwa hapa. Wanafariji nafsi yangu.”

¹⁵⁶ Ni bora kuliko ule upuuzi wote wa kale, hivi vinada vikubwa vya kale vinavyonguruma, vikiendelea, ambapo huwezi hata kula kwenye mikahawa. Ndicho chakula cha Ibilisi. Ni lundo la Ibilisi, lote limechafuliwa na dhambi. Je! nyote mnajumuika kule nje na kufurahia hayo? Wakati wanapoweka fedha hizo kwenye maskini vinanda hivyo, na upuuzi huo wote wa kale unatokea, unafurahia jambo hilo? Huna aibu. Umerudi nyuma. Umeenda mbali na Mungu. Humjui Mungu. Kama ungemjua Mungu, katika msamaha wa dhambi zako, kamwe hungeweza kusikiliza upuuzi kama huo. Ungekuwa umekufa kwako. Unge—ungeutapika. Huutaki. Mlo wako ni bora zaidi. Unampenda Mungu. Mbona usije asubuhi ya leo, upige magoti hapa pamoja na hawa wanaotubu?

¹⁵⁷ Hawa hapa wanaume na wanawake, wanaopiga magoti papa hapa, ambao wamekuwa Wakristo kwa miaka mingi. Mimi siwavui Ukristo. Lakini jambo ninalojaribu kufanya ni

kuwaambia ya kwamba huyo Ibilisi, ambaye anawafuatilia, anawatoa kwenye Furaha iliyo kamili. Roho Mtakatifu ni Furaha. Vema, mimi huamka nikiwa mlevi, ninaenda kitandani mlevi, ninalewa kwa muda mrefu, ni mlevi usiku kucha. Loo, mimi ninaninii—ninapenda tu jambo hilo. Ninaenda kuvua samaki nikiuimba huu, "Usinipite, Ewe Mwokozi mnyenyeketu. Yasikie maombi yangu manyenyeketu." Ninaenda kuwinda, na kuimba sifa za Mungu. Ninahubiri, kila mahali niendako. Hivi hutaki kuwa namna hiyo? Ukipazwa na Roho Mtakatifu, Yeye anakuchangamsha. Loo, jamani! Unawasikia wakiimba hizo nyimba chafu za kale? Unaweza kuuimba:

Ninaelekeea kwenye Nchi ya Ahadi,
 Ninaelekeea kwenye Nchi ya Ahadi;
 Ni nani atakayekuja na kuambatana nami?
 Ninaelekeea kwenye Nchi ya ahadi.

Ninaelekeea kwenye Nchi ya Ahadi,
 Ninaelekeea kwenye Nchi ya Ahadi;
 Ni nani atakayekuja na kuambatana nami?
 Ninaelekeea kwenye Nchi ya ahadi.

Nitaifikia lini ile raha iliyobarikiwa,
 Nipate kubarikiwa milele!
 Nitauna lini uso wa Baba yangu,
 Na kupumzika kifuani Mwake.

Ninaelekeea kwenye Nchi ya Ahadi,
 Ninaelekeea kwenye Nchi ya Ahadi;
 Ni nani atakayekuja na kuambatana nami?
 Ninaelekeea kwenye Nchi ya ahadi.

¹⁵⁸ Mbona usije, uende? Ninakumbuka wakati yapata watu mia tano kati yetu tulipokuwa tumesimama pale hapo nilipokuwa nikibatiza watu mia na ishirini, yapata majira haya ya mwaka, hapa chini ukingoni mwa mto, wakati ile Nyota kuu ya Asubuhi iliposhuka iking'aa kule mtoni. Haleluya! Sauti iliyonena kutoka Kwake, ilisema, "Siku moja utaieneza Injili kila mahali ulimwenguni." Maskini mvulana mdogo, asiyejua kusoma angewezaje kufanya jambo hilo? Hiyo ni neema ya Mungu! Amina.

¹⁵⁹ Loo, ni nani atakayekuja twende? Tupa, weka kando, kila mzigo sasa. Usiwasikilize hao roho wanaoshawishi. Njoo, sikiliza Neno la Mungu, BWANA ASEMA HIVI! "Heri wenye njaa na kiu ya haki, kwa maana watajazwa."

¹⁶⁰ Sasa hebu tuinamishe vichwa vyetu sasa tunapoomba pamoa na hawa waliopo madhabahuni.

Watoto wapendwa, ninataka mkumbuke, asubuhi ya leo, mko hapa kuweka kando kila mzigo. Mko hapa kuweka kando kila mzigo na dhambi iwazingiayo kwa upesi. Paulo alisema, katika Waebrania, sura ya 12.

...kwa kuwa tu-... tumezungukwa na wingu kubwa sana la mashahidi namna hii, na tuweke kando kila mzigo mzito, na dhambi ile... ituzingayo kwa upesi;...

Nami niseme nini tena?... wakati usinge... kuleta habari za Gideoni... Baraka, na Baraka... Samsoni... Yeftha na Daudi... Samweli na za manabii;

Ambao kwa imanini walishinda milki za wafalme, walitenda haki, walipata ahadi, walifunga kinywa cha simba,

Walizima nguvu za moto, waliokoka na makali ya upanga. Walitiwa nguvu baada ya kuwa dhaifu, walikuwa hodari katika vita... waliwakimbiza majeshi ya wageni...

Wanawake walipokea wafu wao waliofufuliwa.

Lakini wengine walipata mateso, wakadhihakiwa vibaya hata kupigwa.... tena, zaidi ya hayo, kwa mafungo, na kwa kutiwa gerezani;

Na—na wengine waliokuwa na majoribu haya... kudhihakiwa na kupigwa...

...wote hao wakiisha kushuhudiwa kwa sababu ya imani yao...

Na watu hao wote wakiisha kushuhudiwa kwa sababu ya imani yao, hawakuipokea ahadi;

Kwa kuwa Mungu alikuwa ametangulia kutuwekea sisi kitu kilicho bora, ili wao wasimkamilike pasipo sisi.

Basi na sisi pia, kwa kuwa tu-... tunazungukwa na wingu kubwa la mashahidi namna hii, na tuweke kando kila mzigo mzito, na dhambi... ituzingiayo kwa upesi; na tupige mbio kwa saburi katika yale mashindano yaliyowekwa mbele yetu,

Tukimtazama Yesu, mwenye kuanzisha na mwenye kutimiza imani yetu; ambaye kwa ajili ya furaha iliyowekwa mbele yake aliustahimili msalaba na kuidharau aibu, na-... ameketi mkono wa kuume wa kiti cha enzi cha Mungu.

¹⁶¹ Yesu, katika ombi Lake, alisema, “Baba, ninajitakasa.” Yesu akatakasika, kwa Kanisa. Yeye angaliweza kuoa, lakini hakufanya jambo hilo. Yeye alitakasika. Alisem, “Watakase, Baba, katika Kweli. Neno Lako ni Kweli.”

¹⁶² Sasa hebu na tuweke kando kila mzigo. Una hamaki? Una jambo fulani, linakufanya uzungumze wakati hupaswi kuzungumza? Ee Mungu! Liweke pale sasa. Liweke pale, angalia Moto wa madhabahu ukishuka na kukiondolea mbali. Angalia upendo wa Mungu ukiilamba. Angalia uchoyo huo wote wa kale, jinsi umekuwa ukizungumza na mkeo, jinsi umekuwa

ukizungumza na mumeo, jinsi umekuwa ukinena na jirani yako, jinsi umekuwa ukinena habari za watu kanisani, yaweke madhabahuni asubuhi ya leo, na Moto wa Mungu utashuka na kuyaondolea mbali mara moja, na upendo wa Kiungu utawako mahali pake.

¹⁶³ Una ugonjwa? Uweke madhabahuni, useme, “Bwana, huu hapa. Niumbie ndani yangu roho iliyo safi. Niumbie ndani yangu nguvu za kuponya.” Uone yale atakayofanya Mungu. Mungu atafanya jambo hilo asubuhi ya leo.

¹⁶⁴ Baba yetu wa Mbinguni, tunainama Mbele Zako, kwa niaba ya hao walio madhabahuni. Jalia neema Yako iwe juu ya kila mmoja wao, Baba. Sasa wakati wao wana-... Bwana, siwezi kufanya jambo hilo kwa ajili yao. Hawana budi kufanya hivyo wao wenyewe. Hakuna mtu anayeweza kufanya jambo hilo kwa ajili yao. Hawana budi kulifanya peke yao. Jalia nafsi zao sasa ziseme ndani yao, “Ee Mungu, hii hapa hamaki, ninaiweka hapa chini, Bwana. Kamwe sitaichukua tena. Hata iweje, nitaachilia, tangu sasa na kuendelea. Ulimi huu wangu ambaو umekuwa ukishiriki vizuri katika makundi ya kusengenyanan, Bwana, ninauweka hapa chini. Sitauchukua tena kamwe. Takasa ulimi wangu, Bwana. Jalia niwasikie Malaika wakipita, kama Isaya alivyowasikia aliposema, ‘Mimi ni mtu mwenye midomo michafu. Ole wangu!’ Ndipo yule Malaika akaja, akachukua koleo, akaenda madhabahuni na kuchukua makaa ya Moto, akayaweka kwenye mdomo wake na kumtakassa. Mungu, mtakase kila mnenaji, asubuhi ya leo, anayenena mabaya na kupanda mbegu za chuki. Tujalie, Bwana.

¹⁶⁵ Magonjwa yote yaliyoinamishwa hapa katika jengo hili, watu walio wagonjwa, tukijua ya kwamba hao ni pepo, pia. Mungu, kama mtumishi Wako, ninawakemea, katika Jina la Yesu. Jalia watoke katika kila mgonjwa. Na jalia kila mtu aliye mchafu, aliye na mawazo machafu, machafu sana, tamaa mbaya, wanawake na wanaume, wote pamoja, Mungu, yaondoe kwao. Hawa wote hapa wanaotaka kuacha sigara, na pombe ndogo za jumuiya, na tafrija ndogo, mambo ya kichoyo; Mungu, uchangamshe moyo wao kwa Roho Mtakatifu hivi kwamba mambo hayo hayatawawutia tena. Hayatakuwa na nafasi yo yote; umejaa sana Roho Mtakatifu, tangu wakati huo na kuendelea.

¹⁶⁶ Mungu, lifanye kanisa hili ndogo kijiti kinachowaka moto. Lifanye kuwa mahali pa Roho Mtakatifu, lifanye Moto unaowaka, ili ulimwengu upate kugeuka kuuona utukufu wa Mungu. Mungu, anza na kundi hili ndogo la watu, la watu mia kadha hapa asubuhi ya leo. Tujalie, Bwana.

¹⁶⁷ Usafishe kila moyo, kila Mmethodisti, kila Mbatisti, kila Mkatoliki, kila Mpresbeteri, kila Mpentekoste. Bwana, litoe moyoni mwao, na wajalie waje Kwako leo. Tujalie, Baba. Ninawakabidhi Kwako, na kuwaweka Kwako, katika Jina la

Yesu Kristo, kwa ajili ya kusafishwa kwa nafsi zao na kuponywa kwa miili yao. Amina.

¹⁶⁸ Sijui, hapa madhabahuni, umeacha mzigo wako? Unajisikia kama uko pale? Kama unajisikia uko pale, wewe kuwa hakimu. Wewe ndiwe unayeomba. Nimemaliza kuhubiri. Wewe omba. Je! mzigo wako umeuacha pale, ndugu, dada? Unaweza kuuacha pale kweli? Kama unaweza, inua mkono wako, useme, “Naam, Mungu, sasa nauacha hapa. Tofauti yangu, nitaicha hapa madhabahuni.” Vipi kuhusu jambo hilo, hapo mwishoni mwa madhabahu, kwenye mkono wangu wa kuume, bibi? Unaweza kuuacha pale? Unaweza kuacha huo mzigo wa kale pale? Useme, “Naam, imani yangu inakutegemea, Ewe Mwana-Kondoo wa Kalvari.” Wakati tunapoimba sote pamoa sasa.

Yesu kwa imani,
Nakutumaini,
Peke Yako;
Nisikie sasa,
Na kunitakasa,
Ni wako kabisa
Tangu leo!

¹⁶⁹ Na tusimame kwa miguu yetu, kwa uchaji sana, kila mmoja. Sasa sikilizeni kwa makini, kila mtu sasa. Mtu ye yote asiondoke. Ninii tu . . . Ibada haijawkwisha. Ninataka mpate utakatifu huu mdogo, uchaji mdogo.

Hapa nazunguka,
Katika mashaka,
Na matata;
Palipo na giza,
Utaniongoza,
Hivi nitaweza
Kufuata.

Usiuimbie jirani wako sasa. Fungeni macho yenu, na hebu tuuimbe pole pole, tunapoinua mikono yetu kwa Mungu.

Hapa nazunguka,
Katika mashaka,
Na matata;
Palipo na giza,
Utaniongoza,
Hivi nitaweza
Kufuata.

Nina Baba huko ng’ambo,
Nina Baba huko ng’ambo,
Nina Baba huko ng’ambo,
Kwenye pwani ya pili.

Loo, siku moja angavu nitaenda kumwona,
 Siku moja angavu nitaenda kumwona,
 Siku moja angavu nitaenda kumwona,
 Kwenye pwani ya pili.

Loo, siku angavu huenda ikawa ni kesho,
 Siku hiyo angavu huenda ikawa ni kesho,
 Siku hiyo angavu huenga ikawa ni kesho,
 Kwenye pwani ya pili.

¹⁷⁰ Sijui sasa, ni wangapi wana baba huko kwenye ile Nchi nyiningine? Hebu tuone mkono wako. Ni wangapi walio na mama kwenye ile Nchi nyiningine? Hebu tuone mkono wako. Ni wangapi walio na Mwokozi kwenye ile Nchi nyiningine? Hebu tuone mkono wako.

Huo si utakuwa ni mukutano wa furaha!
 Huo si utakuwa ni mukutano wa furaha!
 Huo si utakuwa ni mukutano wa furaha!
 Kwenye pwani ya pili.

¹⁷¹ Nawatakeni mfanye jambo fulani. Sasa wakati tunapouimba huo tena, ninataka upeane mikono na mtu fulani anayesimama karibu nawe, na kusema, “Ndugu, dada, niombee, ili kwamba nikutane nawe kwenye ile Nchi nyiningine.” Usifanye jambo hilo isipokuwa uwe unalimaanisha. Ni wangapi wanataka kukutana? Ni wangapi wanaotaka kumkuta kila mtu hapa, Kule? Sisi, sisi tunataka. Sasa hebu tupeane mikono sisi kwa sisi, na kusema, “Ninataka kukutana nawe, ndugu. Ninataka kukutana nawe kwenye ng’ambo ya pili.” Sasa wakati tunapouimba huu, “Nina Mwokozi huko ng’ambo.” Vema.

Nina Mwokozi huko ng’ambo,
 Nina Mwokozi huko ng’ambo,
 Nina Mwokozi huko ng’ambo,
 Kwenye pwani ya pili.

Loo, siku moja angavu nitaenda kumwona,
 Siku moja angavu nitaenda kumwona,
 Siku moja angavu nitaenda kumwona,
 Kwenye pwani ya pili.

¹⁷² Jambo hilo halikufanyi kujisikia vizuri na vema? “Yesu, unihifadhi hapo msalabani.”

Yesu unihifadhi . . .
 Hapo msalabani;
 Wajiao Kalvari,
 Waponywe damuni.

Kila mtu na ainue mkono wake sasa.

Msalaba, msalaba,
 Hapo nina sifa;
 Hata nitapumzika,
 Mahali pa raha.

Msalaba, msalaba,
 Hapo nina sifa;
 Hata nitapumzika
 Mahali pa raha.
 Nampenda, nampenda
 Kwani alinipenda kwanza
 Na kununua wokovu wangu
 Mtini Kalvari.

Mungu asifiwe!

¹⁷³ Hebu tukiwa kimya sasa tuinue mikono yetu. Na katika njia zetu nzuri, hebu na tumshukuru huku tumeinua mikono yetu, tukisema, "Asante, Bwana, kwa kuokoa nafsi yangu. Asante, Bwana, kwa kuniponya. Asante, Bwana, kwa yote uliyofanya, ukituletea ukombozi mzuri, ukituletea wokovu. Asante, Bwana." Tunakupa Wewe dhabihu hizi za shukrani. Tunakusifu kwa sababu Wewe ni mzuri sana. Wewe Ndiwe Ua la Bondeni, Nyota ya Asubuhi, Ua la Uwandani, Uliye Yote katika Yote. Wewe ni Baba, Mwana, Roho Mtakatifu; Yeye aliyekuwako, Aliyeko, na Atakayekuja; yule Alfa mkuu, Omega. Wewe Ndiwe wa Ajabu, Mfalme wa Amani, Mzao wa Kifalme wa Daudi. Wewe ni Yote! Nasi tunakushukuru, Bwana, kwa yote uliyofanya. Tunakushukuru kwa ajili ya Neno Lako, kwa maana ni Nuru katika njia yetu. Loo, tunaomba, Bwana, ya kwamba utatujalia kutembea katika Nuru. Tujalie, Baba. Katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

Vema. Tunapoketi kwa muda kidogo. "Tutatembea Nuruni."

Tutatembea Nuruni, ni Nuru nzuri sana,
 Inakuja ambapo umande wa rehema unang'aa;
 Tumulikie kote, mchana na usiku,
 Yesu, Nuru ya . . .

¹⁷⁴ Njooni, enyi watakatifu, hebu tuuimbe sasa!

Tutatembea Nuruni (usafi, utakatifu), ni Nuru nzuri sana,
 Inakuja ambapo umande wa rehema unang'aa;
 Tumulikie kote, mchana na usiku,
 Yesu, Nuru ya . . .

Njoo, ukamkiri kama Mfalme wako,
 Yesu, Nuru ya ulimwengu;
 Ndipo kengele za Mbinguni zitaimba,
 Yesu, Nuru ya ulimwengu.

Kila mmoja!

Tutatembea Nuruni (Nuru ya njia yangu), ni
 Nuru nzuri sana,
 Inakuja ambapo umande wa rehema unang'aa;
 Tumulikie kote, mchana na usiku,
 Yesu, Nuru ya ulimwengu.

¹⁷⁵ Hilo halikufanyi kujisikia vizuri? Ni wangapi wanaosikia vizuri? Inueni tu mkono wenu sasa, na kusema, “Najisikia vizuri sana.” Roho Mtakatifu alikusafisha kabisa. Kwa hiyo basi (ati nini?) tutatembea Nuruni. Usisikilize ninii yo yote... Nuru ni kitu gani? “Neno Lako ni Taa.” Kwa hiyo basi:

Tutatembea Nuruni, ni Nuru nzuri sana,
Inakuja ambapo umande wa neema unang’aa;
Tumulikie kote, mchana na usiku,
Yesu, Nuru ya...

¹⁷⁶ Sasa, si hilo ni la ajabu sana? Inaonekana tu kana kwamba hatuwezi kumaliza. Roho Mtakatifu ametukamata sana! Hamjisikii namna hiyo? Kujisikia tu kana kwamba haiwezi kuisha. Inaonekana tu kana kwamba hatuwezi kumalizia.

Inatiririka kwa damu,
Damu ya wanafunzi waliokufa kwa ajili ya
Kweli,
Injili hii ya Roho Mtakatifu inatiririka kwa
damu.

Wa kwanza kufa kwa ajili ya mpango huu wa
Roho Mtakatifu,
Alikuwa Yohana Mbatizaji, lakini alikufa
kama mwanamumume;
Ndipo akaja Bwana Yesu, wakamsulibisha,
Yeye alihubiri ya kwamba Roho angewaokoa
watu kutoka dhambini.

Kulikuweko na Petro na Paulo, na Yohana
mtakatifu,
Waliyatoa maisha yao kusudi Injili hii ipate
kuangaza;
Waliichanganya Damu yao, kama wale
manabii wa kale,
Kusudi Neno la Mungu lipate kuhubiriwa kwa
uaminifu.

Ndipo wakampiga Stephano mawe, alihubiri
dhidi ya dhambi,
Akawafanya wakasirike sana, wakakiponda
kichwa chake;
Lakini alikufa katika Roho, akatoa roho yake,
Ndipo akaenda kujiunga na wengine, lile jeshi
lililotoa uhai wao.

Inaendelea kutiririka kwa damu, naam,
inatiririka kwa damu,
Injili hii ya Roho Mtakatifu inatiririka kwa
damu,

Damu ya wanafunzi waliokufa kwa ajili ya
Kweli,
Injili hii ya Roho Mtakatifu inatiririka kwa
damu.

Sikilizeni!

Kuna wale nafsi walio chini ya madhabahu,
wakilia, "Hata lini?"
Bwana apate kuwaadhibu wale waliotenda
maovu;
Lakini kutakuweko na wengine watakaotoa
damu ya uhai wao,
Kwa ajili ya Injili hii ya Roho Mtakatifu
pamoja na mafuriko yake mekundu sana.
Inaendelea kutiririka kwa damu, haleluya,
inatiririka kwa damu,

Ninataka kuwa mmoja wao.

Injili ya Roho Mtakatifu, Inatiririka kwa
damu,
Damu ya wanafunzi waliokufa kwa ajili ya
Kweli,
Injili hii ya Roho Mtakatifu inatiririka kwa
damu.

¹⁷⁷ Ningetaka kwenda moja kwa moja kutoka madhabahuni. Amina. Loo, ni ajabu jinsi gani! Ndugu zangu walitoa damu ya maisha yao. Kutakuweko na wengine watakaofanya jambo lile lile. Msihofu. Inaelekea kwenye shindano la kuamua hivi karibuni sana. Aidha utaingia ndani au utatoka nje. Wote wamejiandikisha sasa kwenye Baraza la Makanisa, na wote wanaingia. Wote wanakusayika pamoja.

Na kutakuweko na wengine watakaotoa damu
ya uhai wao,
Kwa ajili ya Injili hii ya Roho Mtakatifu
pamoja na mafuriko yake mekundu sana.
Inatiririka kwa damu, naam, inatiririka, (Loo,
haleluya!)
Injili hii ya Roho Mtakatifu inatiririka kwa
damu,
Damu ya wanafunzi waliokufa kwa ajili ya
Kweli,
Injili hii ya Roho Mtakatifu, Inatiririka kwa
damu.

¹⁷⁸ Jamani! Ninajisikia kana kwamba Kunyakuliwa kuko tu juu ya kanisa. Loo, linanifanya nijisikie vizuri sana! Dhambi zote zimo chini ya Damu. Mnaona, Roho Mtakatifu analipenda Neno. Neno ndilo Roho Mtakatifu analojilisha, mnaona. Loo, jamani! Linashuka na kuwa mionganoni mwa watu, linawasafisha

dhambi zao, na kundolea mbali magonjwa yao, linaondolea mbali huzuni zao. Sasa mimi nimelewa, nimelewa tu niwezavyo kuwa, nimelewa kwa Roho, huku upendo ukitoka moyoni mwangu. Haidhuru mtu ye yote amewahi kufanya jambo gani, amesamehewa. Adui wako mbaya sana, yote yamekwisha. Mtu ye yote aliywahi kunena ama kusema jambo lo lote, kama mimi . . . vema, mimi . . . yote yamekwisha, yameoshwa sasa.

Na inatiririka kwa damu, naam, inatiririka,
Injili ya Roho Mtakatifu inatiririka kwa damu,
Damu ya wanafunzi waliokufa kwa ajili ya
Kweli,
Injili hii ya Roho Mtakatifu . . .

Lo, jamani! Ni ajabu jinsi gani!

Ni wakati wa ajabu viyi kwako,
Ni wakati wa ajabu viyi kwangu;
Kama sote tukijitayarisha kumlaki Yesu
Mfalme wetu,
Utakuwa ni wakati wa ajabu jinsi gani.

Ni wakati wa ajabu viyi kwako,
Ni wakati wa ajabu viyi kwangu;
Kama sote tukijitayarisha kumlaki Yesu
Mfalme wetu,
Utakuwa ni wakati wa ajabu jinsi gani.

Mnapenda jambo hilo? Kila mtu, hima!

Ni wakati wa ajabu viyi kwako,
Ni wakati wa ajabu viyi kwangu;
Kama sote tukijitayarisha kumlaki Yesu
Mfalme wetu,
Utakuwa ni wakati wa ajabu jinsi gani.

¹⁷⁹ Ninajisikia tu kana kwamba ufufuo wa mtindo wa kale umo kanisani. Nawe je! Na kusafishwa kwa mtindo wa kale tu, kusafishwa kabisa; wakati mzuri, wa mtindo wa kale. Hamjisikii vizuri? Loo!

Nitamsifu, nitamsifu,
Nitamsifu Mwana-Kondoo aliyechinjwa kwa
ajili ya wenye dhambi.

Na tuuimbe sasa, kila mtu. Mnaoujua? Ninaujua. Njoo hapa; nisaidie kuuongoza, Ndugu Neville. Nanyi nyote, pamoja, inueni mikono yenu, imbeni pamoja na mimi sasa, sasa, asubuhi ya leo.

Msifuni Mwana-Kondoo aliyechinjwa kwa
ajili ya wenye dhambi;
Mpeni sifa, enyi watu wote,
Kwa maana Damu Yake imeosha kila waa.

¹⁸⁰ Sasa, kila mtu, shime!

Nitamsifu, nitamsifu,
 Nitamsifu Mwana-Kondoo aliyechinjwa kwa
 ajili ya wenyе dhambi.
 Mpeni sifa enyi watu wote,
 Kwa maana damu Yake imeosha kila waa.

Amina. Huo ni mzuri sana?

Lango jeupe la lulu,
 Nina jumba kubwa, kinubi, na taji;
 Sasa ninangojea, ninakesha na kuomba,
 Kwa ajili ya ule Mji alionuona Yohana ukishuka.

¹⁸¹ Amina. Ni mzuri sana! Loo! Sasa na tusimame kwa miguu yetu, kila mmoja. Natumaini mnajisikia vizuri. Kumbukeni ibada usiku wa leo. Sasa tunataka kuimba wimbo wetu mzuri wa kupumukana.

Kwa Jina la Bwana Yesu,
 Ninajinamisha;
 Ndiye Mfalme wa wafalme
 Hakika ya maisha.

Vema. Kila mmoja sasa, pamoja. Vema.

Kwa Jina la Bwana Yesu,
 Ninajinamisha;
 Ndiye Mfalme wa wafalme
 Hakika ya maisha.

Dhamani (dhamani), na tamu, (na tamu!)
 Ni Jina Lake Yesu
 Dhamani (dhamani), na tamu! (na tamu!)
 Ni Jina Lake Yesu.

¹⁸² Ni asubuhi ya ajabu jinsi gani! Ni wakati mzuri namna gani! Hebu tuinamishe vichwa vyetu sasa kwa muda kidogo tu. Kila mtu na aangalie moja kwa moja kwa Kristo sasa, Mwokozi wenu. Kwa unyamavu, ninataka kumpa Yeye shukrani na sifa. Kusema, "Bwana, ninakushukuru sana kwa kuitakasa nafsi yangu. Ninakushukuru sana kwa yote uliyonitendea. Jalia Roho Wako awe juu yangu siku nzima, Bwana. Niongoze. Nielekeze. Nibariki." Mungu na akujalilie baraka hiyo, ndilo ombi langu.

Sasa wakati tukiinamisha vichwa vyetu, Ndugu Neville, turuhusu tupumukane katika maombi.



Elimu Juu ya Pepo — Milki ya Kimwili
8 Juni, 1953, Jumatatu alasiri
Roberts Park Amphitheater, Connersville, Indiana

Elimu Juu ya Pepo — Milki ya Kidini
9 Juni, 1953, Jumanne alasiri
Roberts Park Amphitheater, Connersville, Indiana

Roho Zinazoshawishi
24 Julai, 1955, Jumapili asubuhi
Maskani Ya Branham, Jeffersonville, Indiana

Jumbe hizi za Ndugu William Marrion Branham, zilizohubiriwa hapo awali katika Kiingereza, zimetolewa kwenye kanda za sumaku zilizorekodiwa na kuchapishwa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice of God Recordings. Ilachapishwa tena katika mwaka wa 2013.

SWAHILI

©2001 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org